



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA
JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (MB), WAZIRI WA MAMBO YA
NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIPIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA
KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**



Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akikabidhiwa Uenyekiti wa SADC na Mheshimiwa Dkt. Hage Geingob, Rais wa Jamhuri ya Namibia jijini Dar es Salaam mwezi Agosti 2019.



Mhe. Prof. Palamagamba J.A.M Kabudi (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki akimshukuru Mhe.Tehindrazanarivelo Djacoba A.S Oliva, Waziri wa Mambo ya Nje wa Madagascar baada ya kukabidhiwa zawadi ya dawa ya Homa Kali ya Mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19).



Mhe. Prof. Palamagamba J. A. M. Kabudi (Mb),
WAZIRI



Mhe. Dkt. Damas D. Ndumbaro (Mb),
NAIBU WAZIRI



Balozzi Kanali Wilbert A. Ibuge,
KATIBU MKUU



Balozzi Ramadhan M. Mwinyi,
NAIBU KATIBU MKUU

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA
JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (MB), WAZIRI WA
MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA
MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO
YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA
MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI CHA SERIKALI YA AWAMU YA TANO	7
3.0 MISINGI YA TANZANIA KATIKA MAHUSIANO YA KIMATAIFA	20
4.0 TATHMINI YA HALI YA DUNIA KWA MWAKA 2019/2020	21
4.1 Hali ya Uchumi Duniani.....	21
4.2 Hali ya siasa, ulinzi na usalama.....	24
5.0 NAFASI YA TANZANIA KIMATAIFA NA KIKANDA....	47
6.0 KUJENGA NA KULINDA TASWIRA YA NCHI KIMATAIFA	53
7.0 WATANZANIA KWENYE NAFASI ZA KIMATAIFA	58
8.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020	62
8.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje	66
8.1.1 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Afrika.....	66
8.1.2 Ushirikiano kati ya Tanzania na Nchi za Asia na Australasia	71
8.1.3 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Mashariki ya Kati	81
8.1.4 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Ulaya na Amerika	86
8.1.5 Ushirikiano wa Kikanda.....	92
8.1.6 Ushirikiano wa Ubia Kati ya Tanzania na Nchi Nyingine	128
8.1.7 Ushirikiano wa Kimataifa.....	133
8.2 Kufuatilia na Kusimamia Utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa	137

8.3	Kuratibu Mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano na Kufuatilia Utekelezaji wa Makubaliano	141
8.4	Masuala ya Diplomasia, Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli	144
8.4.1	Kuratibu Ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Nje ya Nchi.....	144
8.4.2	Kuratibu Ziara za Viongozi wa Kitaifa na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa kutoka Nje ya Nchi	147
8.5	Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli.	149
8.6	Ushirikishwaji wa Watanzania wanaoishi ughaibuni	151
8.7	Elimu kwa Umma	154
8.8	Mpango Mkakati wa Wizara kwa Kipindi cha Mwaka 2020/2021- 2024/2025	155
8.9	Utawala na Maendeleo ya Watumishi.....	155
8.9.1	Uteuzi wa Viongozi	156
8.9.2	Mafunzo	156
8.9.3	Upandishaji Vyeo Watumishi	157
8.9.4	Uhamisho	157
8.9.5	Umiliki wa majengo	158
8.10	Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi zilizo Chini ya Wizara	159
8.10.1	Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara.....	159
8.10.2	Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara.....	160
9.0	CHANGAMOTO ZILIZOPO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA	167
10.0	SHUKRANI	169

11.0	MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021	175
12.0	MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021	178
13.0	MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021	180
14.0	HITIMISHO	183

ORODHA YA VIFUPISHO

AfCFTA	African Continental Free Trade Area
AfDB	African Development Bank
AICC	Arusha International Conference Centre
AMISOM	The African Union Mission in Somalia
APRM	African Peer Review Mechanism
AU	African Union
BADEA	Arab Bank for Economic Development
CFR	Centre for Foreign Relations
COMESA	Common Market for Eastern and Southern Africa
COVID – 19	Corona Virus Disease 2019
CPC	Communist Party of China
DRC	Democratic Republic of Congo
EAC	East African Community
EADB	East African Development Bank
EPZA	Export Processing Zone Authority
FAO	Food and Agriculture Organization of the United Nations

FOCAC	Forum on China – Africa Cooperation
IAEA	International Atomic Energy Agency
ICGLR	International Conference on the Great Lakes Region
IFAD	International Fund for Agricultural Development
ILO	International Labour Organization
IMF	International Monetary Fund
IOM	International Organisation for Migration
IORA	Indian Ocean Rim Association
JKCI	Jakaya Kikwete Cardiac Institute
JNIA	Julius Nyerere International Airport
JNICC	Julius Nyerere International Convention Centre
KCMC	Kilimanjaro Christian Medical Centre
KfW	German Development Bank
KIA	Kilimanjaro International Airport
MSD	Medical Stores Department
MINUSCA	United Nations Multidimensional Integrated Stabilisation Mission in Central African Republic

MONUSCO	United Nations Organization Stabilisation Mission in the Democratic Republic of Congo
OACPS	Organization of Africa, Caribbean and Pacific States
OSBP's	One-Stop Border Posts
PAIGC	Political Party for the Independence of Guinea and Cabo Verde
PAPU	Pan African Postal Union
RENAMO	Resistência Nacional Moçambicana (Mozambican National Resistance)
SADC	Southern African Development Community
STAMICO	State Mining Corporation
TANTRADE	Tanzania Trade Development Authority
TAZARA	Tanzania - Zambia Railways Authority
TCCIA	Tanzania Chamber of Commerce Industry and Agriculture
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TICAD	Tokyo International Conference on African Development
TIC	Tanzania Investment Centre

TRC	Tanzania Railways Corporation
UAE	United Arab Emirates
UKIMWI	Ukosefu wa Kinga Mwilini
UNAIDS	Joint United Nations Programme on HIV and AIDS
UNAMID	African Union and United Nations Hybrid Operation in Darfur
UNCDF	United Nations Capital Development Fund
UNCTAD	United Nations Conference on Trade and Development
UNDP	United Nations Development Programme
UNEP	United Nations Environment Programme
UNESCO	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
UNFIL	United Nations Interim Force in Lebanon
UNFPA	United Nations Population Fund
UNHCR	United Nations High Commissioner for Refugees
UNISFA	United Nations Interim Security Force for Abyei
UNICEF	United Nations Children's Fund

UNIDO	United Nations Industrial Development Organization
UNMISS	United Nations in the Republic of South Sudan
UNRCO	United Nations Resident Coordinator Office
UNODC	United Nations Office on Drugs and Crime
UN Women	United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women
VVU	Virusi Vya Ukimwi
WIOMSA	Western Indian Ocean Marine Science Association
WFP	World Food Programme
WHO	World Health Organization

1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniruzuku uhai na kunijalia afya njema ya kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inahitimisha ngwe yake ya kwanza ya miaka mitano mwaka huu, niruhusu kwa namna ya kipekee kabisa kumpongeza, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri ambao umeliletea Taifa hili maendeleo makubwa katika kipindi hiki cha uongozi wake. Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza vyema nchi yetu na kutekeleza kwa mafanikio makubwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020.

4. Mheshimiwa Spika, mtakuwa mashahidi kwamba chini ya uongozi wa viongozi wetu hawa mahiri nchi yetu imepiga hatua kubwa sana kimaendeleo ikiwemo kutekeleza miradi muhimu ya maendeleo. Aidha, dira na maono ya viongozi wetu hawa imeifanya nchi yetu kuendelea kuwa ya amani na utulivu na Watanzania tumeendelea kudumisha mshikamano na umoja wa kitaifa, na hapana shaka tumeendelea kuwa mfano wa kuigwa kwa nchi nyingine za Afrika na duniani kote.

5. Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, ninawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni.

6. Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri na uongozi wake madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb), Naibu Spika; Wenyeviti wa Bunge; na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri wanazozifanya kumsaidia Spika katika kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge. Naomba Mwenyezi Mungu azidi kuwajaalia afya njema, busara na hekima katika kuongoza mhimili huu muhimu katika Taifa letu.

7. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mheshimiwa Salim Mwinyi Rehani (Mb), kwa kazi nzuri na ya kizalendo inayoifanya ya kuishauri Serikali hususan Wizara yangu. Aidha, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi kirefu. Naomba nikiri kuwa miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali umekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

8. Mheshimiwa Spika, naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki kwa kuchaguliwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2019/2020. Kuchaguliwa kwake ni kielelezo cha kuaminiwa na wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki katika kuwaletea maendeleo.

9. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa jimbo la Newala Vijijini kwa kifo cha Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar

aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo kilichotokea tarehe 15 Januari 2020. Vilevile, napenda kutoa pole kwako na Bunge lako Tukufu kwa kifo cha Mheshimiwa Askofu Dkt. Getrude Rwakatare, (Mb), kilichotokea tarehe 20 Aprili 2020.

10. Mheshimiwa Spika, pia naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa jimbo la Sumve kwa kifo cha Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo kilichotokea tarehe 29 Aprili 2020. Kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga (Mb), aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na kabla ya hapo Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kilichotokea tarehe 1 Mei 2020.

11. Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kuwa vifo hivi ni pengo kubwa kwa Taifa kutokana na michango yao adhimu katika kulitumikia Taifa hili. Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi. Amina.

12. *Mheshimiwa Spika*, kimataifa pia kulitokea misiba ya viongozi mbalimbali ambayo Serikali ilituma salamu za rambirambi na kutuma wawakilishi. Kwa mara nyingine tena, kwa niaba ya Serikali naomba kutoa salamu za pole kwa ndugu zetu wa Jamhuri ya Kenya kwa kifo cha Hayati Daniel Toroitich Arap Moi, Rais Mstaafu wa nchi hiyo; ndugu zetu wa Jamhuri ya Zimbabwe kwa kifo cha Muasisi wa Taifa hilo Hayati Robert Gabriel Mugabe; ndugu zetu wa Jamhuri ya Misri kwa kifo cha Hayati Hosni Mubarak, Rais Mstaafu wa nchi hiyo; ndugu zetu wa Oman kwa kifo cha Muadham Sultan Qaboos Bin Said al Said; ndugu zetu wa Tunisia kwa kifo cha Hayati Beji Caid Essebsi, aliyekuwa Rais wa nchi hiyo; na ndugu zetu wa Ufaransa kwa kifo cha Hayati Jacques Chirac, Rais Mstaafu wa nchi hiyo. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi. Amina.

13. *Mheshimiwa Spika*, vilevile naomba kutoa salamu za pole kwa Serikali za nchi zilizokumbwa na mashambulizi ya kigaidi yakiwemo yaliyotokea katika Ukanda wa Pembe ya Afrika, Ukanda wa Sahel, Ukanda wa Bonde la Mto Chad na sehemu ya Kusini mwa Afrika. Mashambulizi hayo yamesababisha vifo, ulemavu na uharibifu wa mali. Tanzania inaungana na mataifa mengine

duniani kukemea na kulaani vikali vitendo hivyo vya kikatili dhidi ya binadamu.

2.0 MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI CHA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

14. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya mwisho nikiwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano, ninayo heshima kuelezea kwa ufupi baadhi ya mafanikio makubwa ambayo Wizara inajivunia kuyaratibu kwa ufanisi mkubwa na kufanikisha utekelezaji wake kwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano kama ifuatavyo:

- i) Ufunguzi wa balozi mpya nane za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi za Qatar; Uturuki; Sudan; Cuba; Israel; Algeria; Jamhuri ya Korea; na Namibia. Kufunguliwa kwa Balozi hizo, kunaifanya Tanzania kuwa na jumla ya Balozi 43 na Konseli Kuu tatu katika miji ya Mombasa, Dubai na Jeddah. Kadhalika, Balozi za Ethiopia na Poland zilifunguliwa hapa nchini katika kipindi hicho na kuifanya Tanzania kuwa mwenyeji wa Balozi 62 na Mashirika ya Kimataifa 30;

ii) Tumefanya jitihada kubwa katika kuifanya lugha ya Kiswahili kutumika katika Jumuiya ya Kimataifa na nchi mbalimbali. Juhudi hizo za Tanzania zimefanya Kiswahili kitumike katika eneo la Maziwa Makuu, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na vyombo mbalimbali vya habari vya Kimataifa.

iii) Kufanikisha kufanyika kwa viwango vya juu Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika Dar es Salaam mwezi Agosti 2019 ambapo Tanzania ilikabidhiwa rasmi Uenyekiti wa Jumuiya hiyo utakaodumu kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi Agosti 2020. Katika uenyekiti wetu wa SADC, tumefanikiwa mambo makuu yafuatayo:

a) Kushawishi na kufanikiwa kupitishwa kwa lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne ya SADC kwa kutambua lugha ya Kiswahili ni lugha ya ukombozi Kusini mwa Afrika iliyotumika wakati wa mapambano ya kuzikomboa nchi hizo kutoka katika ukoloni na utawala wa ubaguzi wa rangi wa Afrika Kusini. Aidha, katika kukuza lugha yetu ya Kiswahili kwenye Jumuiya ya Afrika

Mashariki mitaala ya kufundishia lugha hiyo imeandaliwa na kuanza kutumika;

b) Kufanikiwa kuzishawishi Nchi Wanachama wa SADC kukubaliana na azimio la kutenga tarehe 25 Oktoba ya kila mwaka kuwa siku maalum ya kupaza sauti ya pamoja kwa nchi za SADC, kuzitaka Marekani na baadhi ya Nchi Wanachama za Jumuiya ya Ulaya kuiondolea nchi ya Zimbabwe vikwazo vya kiuchumi vya muda mrefu mpaka hapo vitakapoondolewa;

c) Kufanikiwa kuzishawishi Nchi Wanachama wa Jumuiya ya nchi za Afrika, Karibeani na Pasifiki (OACPS) kuunga mkono jitihada za SADC katika kuhimiza vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa dhidi ya Zimbabwe kuondolewa. Nchi za OACPS ziliunga mkono kwa kauli moja wito wa kuondolewa vikwazo dhidi ya Zimbabwe kwa kujumuishwa kwenye maazimio ya Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya nchi za Afrika, Karibeani na Pasifiki (OACPS) uliofanyika mwezi Desemba, 2019 Jijini Nairobi, Kenya; na

- d) Kuwa mwenyeji wa maadhimisho ya Maonesho ya Awamu ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambayo yalifanyika mwezi Agosti 2019. Lengo la Maonesho hayo lilikuwa ni kuwawezesha wafanyabiashara wa nchi za SADC kutangaza bidhaa zao kwa lengo la kupanua soko ndani ya Jumuiya hiyo. Vilevile, kupitia Maonesho hayo, wafanyabiashara walipata fursa ya kubadilishana uzoefu wa namna ya kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya Jumuiya hiyo. Maonesho hayo yalishirikisha wajasiriamali wapatao 5,352 kutoka ndani na nje ya nchi, Taasisi za umma, viwanda mbalimbali, Taasisi za huduma za fedha na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda.
- iv) Wizara imefanikiwa kuhamasisha watalii kuja nchini kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2015 hadi 2018, watalii 5,234,448 wametembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini. Watalii hao walitoka nchi mbalimbali zilizopo Bara la Afrika; Ulaya; Amerika ya Kaskazini; Asia; Mashariki ya Kati; Australasia na nchi za Karibeani;

- v) Kuratibu ujio wa Madaktari Bingwa wa fani tofauti kutoka nchi mbalimbali kama vile: Umoja wa Falme za Kiarabu; Saudi Arabia; Misri; Israel; Italia; China; India; Pakistan; Marekani; Ujerumani na Cuba. Madaktari hao walitoa huduma za kitabibu katika baadhi ya hospitali zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar na kufanikisha msaada wa ujenzi wa jengo la Kitengo cha Magonjwa ya Dharura katika Hospitali ya Benjamin William Mkaapa iliyopo jijini Dodoma.
- vi) Kuratibu ushiriki wa Tanzania katika kurejesha na kuimarisha amani na utulivu kwa kushiriki katika utatuzi wa migogoro na operesheni za kulinda amani kikanda na kimataifa. Hadi sasa Tanzania ina jumla ya walinda amani 2,303 kwenye misheni sita za kulinda amani za Umoja wa Mataifa kama ifuatavyo: MINUSCA 455, MONUSCO 969, UNAMID 686, UNIFIL 159, UNISFA 12 na UNIMISS 22;
- vii) Kuratibu ziara za Wakuu wa Nchi na Serikali mbalimbali wanaokuja nchini ambapo pia husaini Makubaliano ya Ushirikiano katika Sekta mbalimbali zikiwemo za kilimo, utalii, afya, uwekezaji, usafiri wa anga na

utamaduni. Ziara hizo zina umuhimu mkubwa kwenye kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia, pia Makubaliano hayo yana faida kubwa katika maendeleo ya sekta husika na nchi kwa ujumla;

viii) Kuratibu na kushiriki katika mikutano 12 ya Tume za Pamoja za Ushirikiano kati ya Tanzania na nchi za Kenya, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Uganda (mikutano mitatu), Zimbabwe, Namibia, Misri, Umoja wa Falme za Kiarabu na Uturuki. Mikutano hiyo imewezesha Serikali yetu kufikia makubaliano na nchi hizo katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano kwa manufaa ya Taifa letu;

ix) Kuratibu na kufanikisha ziara za kimataifa za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Baadhi ya ziara za viongozi hao zilifanyika katika nchi za Kenya, Rwanda, Uganda, Malawi, Afrika Kusini, Namibia, Zimbabwe, Misri, Ethiopia, China, Djibout,

Indonesia, India, Jordan, Mauritius, Niger, Angola, Eswatini, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi, Canada, Uingereza, Cuba na Japan. Ziara hizi zimekuwa na mafanikio makubwa katika kuimarisha mahusiano yetu na nchi hizo. Aidha, nchi ilipata fursa mbalimbali za ushirikiano wa kimaendeleo kupitia ziara hizo;

- x) Kufanikisha uenyekiti wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo mwezi Machi 2016 nchi yetu iliteuliwa kwa mara ya pili mfululizo kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo. Katika kipindi cha uenyekiti wake, Tanzania ilifanikisha utekelezaji wa masuala mbalimbali ikiwemo:
 - a) Kuweka mifumo bora ya matumizi ya rasilimali za Jumuiya;
 - b) Kuimarisha miundombinu yenye sura ya Kikanda;
 - c) Kuweka mazingira wezeshi ya kibiashara kwa Nchi Wanachama;
 - d) Kuratibu utumiaji wa Bendera ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Ofisi zote za Umma nchini; na

e) Matumizi ya Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Taasisi zote za Serikali.

xi) Kuratibu Mkutano wa 18 wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Afrika na Nordic (Africa - Nordic Summit) uliofanyika kwa mafanikio makubwa mwezi Novemba 2019 jijini Dar es Salaam. Ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano huo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2001. Tofauti na mikutano iliyopita mkutano huu ulijikita katika kuimarisha masuala ya biashara, uwekezaji, uchumi wa viwanda, mazingira, kukuza utalii pamoja na masuala ya amani na usalama;

xii) Kuratibu ujenzi wa vituo vinane vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani (OSBPs) ambapo vituo saba vipo katika mipaka ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kituo kimoja kipo mpakani mwa Tanzania na Zambia. Uwepo wa vituo hivyo, umerahisisha ufanyaji wa biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za jirani;

xiii) Kufanikisha ujumuishwaji wa miradi ya Tanzania katika miradi ya kipaumbele ya miundombinu iliyoidhinishwa na Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo

baadhi yake ni ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA Terminal III) uliokamilika; barabara ya Kikanda ya Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5); mradi wa ujenzi, upanuzi na ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam zenye zaidi ya km 43 na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA); uwanja wa ndege wa Karume; na bandari za Zanzibar ikiwemo Maruhubi;

xiv) Katika kipindi cha mwaka 2015 – 2019, Tanzania ilifanikiwa kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja za Jumuiya ya Afrika Mashariki kama vile:

a) Kuondoa vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha 15 kati ya vikwazo 24 vilivyoripotiwa dhidi ya Tanzania;

b) Kutoa vyeti 32,536 vya uasili wa bidhaa kwa wafanyabiashara wa Tanzania wanaofanya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki;

- c) Kutoa vibali vya kuingia nchini 1,117,056 kwa raia wa Nchi Wanachama wa Jumuiya na wananchi wetu 851,470 walipata vibali vya kuingia katika nchi nyingine za Jumuiya;
- d) Kufanikisha Watanzania 1,555 kupata vibali vya kufanya kazi katika nchi nyingine wanachama wa Jumuiya na Tanzania ilitoa vibali 2,309 vya kufanya kazi nchini kwa raia wengine wa Nchi Wanachama wa Jumuiya;
- e) Kutoa vibali vipatavyo 879 kwa wanafunzi wa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya kuingia na kusoma nchini na wanafunzi Watanzania 3,129 walipata vibali vya kusoma katika Nchi Wanachama wa Jumuiya; na
- f) Kutoa vibali vya ukaazi 3,128 kwa raia wengine wa Nchi Wanachama wa Jumuiya na Watanzania 1,002 walipata vibali vya ukaazi katika Nchi Wanachama wa Jumuiya.

xv) Kuendelea kuhakikisha kuwa Tanzania inanufaika ipasavyo na fursa za kibiashara

zitokanazo na uanachama wetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi cha mwaka 2015-2018, thamani ya mauzo ya Tanzania katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki iliongezeka kutoka Dola za Marekani **350,169,250** mwaka 2015 na kufikia Dola za Marekani **448,644,006** mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 28. Thamani ya ununuzi wa bidhaa kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya imeongezeka kutoka Dola za Marekani **227,216,173** mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Marekani **302,728,624** mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 33.

xvi) Kuratibu mchakato wa upatikanaji wa Kampuni za *Arab Contractors na El Sewedy Electric* za Misri kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Megawati 2,115 katika Bonde la mto Rufiji (Mwalimu Julius Nyerere Hydropower Project). Ujenzi wa mradi huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Julai, 2019. Aidha, itakumbukwa kuwa mwaka 2017 wakati Tanzania ilipokuwa mwanachama wa Kamati ya Urithi wa Dunia (World Heritage Committee) ya UNESCO, Serikali yetu ilijulisha rasmi Kamati hiyo wakati wa Mkutano wake wa 41

azma ya Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Maguli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kutekeleza mradi huo mkubwa;

xvii) Kuratibu upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato jijini Dodoma na upatikanaji wa mkopo wenye masharti nafuu wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 180 kutoka Benki hiyo kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya pete katika jiji la Dodoma. Ujenzi wa barabara hiyo utasaidia kuboresha miundombinu na kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dodoma;

xviii) Kuratibu upatikanaji wa Kampuni ya SENER ya Korea Kusini kwa ajili ya kujenga meli mpya ya kisasa katika Ziwa Victoria yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo; ujenzi wa Chelezo na ukarabati wa meli za MV Victoria na MV Butiama. Ujenzi wa meli mpya unatekelezwa kwa ubia kati ya kampuni ya Korea Kusini kwa kushirikiana na SUMA JKT na unatarajiwa kukamilika mwaka 2021;

xix) Kuratibu upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa daraja jipya la Selander jijini Dar es Salaam lenye urefu wa kilomita 1.03. Mkopo huo kutoka Serikali ya Korea Kusini ni Shilingi Bilioni 556.5 wakati Serikali ya Tanzania inachangia kiasi cha Shilingi Bilioni 266 ambazo ni fedha za ndani za walipa kodi. Ujenzi wa daraja hilo, utajumuisha barabara za maungio zenye urefu wa kilomita 5.2 na hivyo kufanya mradi mzima kuwa na kilomita 6.23, mradi utagharimu Dola za Marekani Milioni 126.26; na

xx) Kushawishi nchi marafiki kutufutia madeni, kuyapunguza au kuweka masharti nafuu ya kuyalipa. Kutokana na ziara ya Mhe. Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki nchini Iran mwezi Oktoba 2017, Serikali ya nchi hiyo iliridhia na kutangaza kusamehe riba ya deni lililokopwa mwaka 1984 ambayo ilifikia kiasi cha Dola za Marekani Milioni 150. Vile vile, mwezi Septemba 2017, Serikali ya Brazil pia ilitoa msamaha wa thamani ya Dola za Marekani Milioni 203.6 ambayo ni asilimia 86 ya deni lote tunalodaiwa na nchi hiyo. Misamaha hiyo ni wazi itaipa nafuu nchi yetu katika kulipa madeni na

kuelekeza fedha hizo katika maeneo mengine ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

3.0 MISINGI YA TANZANIA KATIKA MAHUSIANO YA KIMATAIFA

15. *Mheshimiwa Spika*, historia ya Tanzania imesheheni misingi na misimamo imara inayoifanya iendelee kuwa miongoni mwa nchi zilizo na ushawishi mkubwa kikanda na kimataifa tangu Uhuru. Misingi ya nchi yetu kuheshimika kimataifa iliwekwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alikuwa mstari wa mbele katika kulaani ubabe, uonevu na ukandamizaji popote pale ulipotokea duniani na alipigania uhuru wa Afrika na kuisisitiza mshikamano kati ya nchi zinazoendelea. Kupitia misingi hii ambayo viongozi wetu wameendelea kuienzi, Tanzania imeendelea kuheshimika sana kikanda na kimataifa.

16. *Mheshimiwa Spika*, katika kusimamia misingi hiyo, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kulinda uhuru wa nchi, haki yetu ya kujiamulia mambo yetu wenyewe bila kuingiliwa, mipaka ya nchi yetu; kuimarisha ujirani mwema; na kutekeleza Sera ya Kutofungamana na Upande Wowote kama dira na msimamo wetu

kwenye mahusiano na nchi nyingine za Jumuiya ya Kimataifa. Kwa muktadha huo, Tanzania imeendelea kushiriki katika kulinda amani, kudumisha umoja na mshikamano, kuhimiza maendeleo na kupinga dhuluma.

17. *Mheshimiwa Spika*, napenda kutoa wito kwa Jumuiya ya Kimataifa kuendeleza ushirikiano katika kutokomeza umaskini, kuboresha utoaji wa huduma za kijamii, kiwango cha elimu, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kudumisha amani na usalama, kuleta haki na kuifanya dunia kuwa sehemu salama ya kuishi.

4.0 TATHMINI YA HALI YA DUNIA KWA MWAKA 2019/2020

18. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa taarifa fupi kuhusu hali ya dunia kama ifuatavyo:

4.1 Hali ya Uchumi Duniani

19. *Mheshimiwa Spika*, hadi mwanzoni mwa mwaka 2020, uchumi wa dunia ulionesha kuendelea kuimarika na kutoa matumaini ya kuimarika zaidi kwa kipindi cha miaka michache ijayo. Uimara wa uchumi katika mataifa makubwa na nchi zinazoibukia kiuchumi uliongeza

upatikanaji wa mitaji, kuimarika kwa bei ya bidhaa na kukua kwa biashara ya kimataifa. Nchi za kusini mwa jangwa la Sahara, ikiwemo Tanzania, zilitarajiwa kunufaika zaidi na mwenendo huo wa uchumi wa dunia. Hata hivyo, mlipuko wa maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19) unaashiria tishio kubwa la kuporomoka kwa uchumi wa dunia.

20. *Mheshimiwa Spika*, ni matumaini yetu kuwa Jumuiya ya Kimataifa itaendelea kushirikiana kwa karibu ili kusaidia juhudi za kukabiliana na janga hili. Kadhalika, ni muhimu kwa Jumuiya ya Kimataifa kusaidia nchi zinazoendelea ili kuimarisha sera za kiuchumi na fedha na kuweka mifumo madhubuti ya kukabiliana na madhara ya kiuchumi yatakayotokana na COVID-19.

21. *Mheshimiwa Spika*, hivi karibuni kumeibuka mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19) ulioripotiwa kwa mara ya kwanza mwezi Desemba 2019 katika mji wa Wuhan, Jimbo la Hubei nchini China na kusababisha vifo, taharuki na athari kubwa za kiuchumi duniani. Aidha, ugonjwa huo umekuwa ukienea kwa kasi kubwa kutoka nchi moja hadi nyingine ambapo kwa

mujibu wa Shirika la Afya Duniani hadi kufikia **tarehe 5 Mei 2020** takribani watu **3,525,116** kote duniani walibainika kuwa na maambukizo ya ugonjwa huo na watu takribani **243,540** walikuwa wamepoteza maisha.

22. Mheshimiwa Spika, athari za ugonjwa wa COVID-19 kwenye sekta zote za uchumi zinakadiriwa kuwa kubwa sana. Taarifa ya mwezi Aprili 2020 iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kuhusu hali ya uchumi duniani pamoja na taarifa ya Benki ya Dunia kuhusu athari za COVID-19 kwenye uchumi wa Afrika, zinaashiria kuwa kuna uwezekano mkubwa uchumi wa dunia kuporomoka kwa kiwango kibaya kinachoweza kulinganishwa na mdodoro wa uchumi wa dunia uliotokea miaka ya 1929 hadi 1933 (*Great Depression*). Tishio hili linatarajiwa kuathiri bei za bidhaa, kupunguza uzalishaji viwandani, kuathiri upatikanaji wa mitaji, ajira na kudorora kwa uwekezaji wa Kimataifa.

23. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuliomba Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuchukua tahadhari zote muhimu za kujikinga na maambukizi ya virusi vinavyosababisha ugonjwa huu kwa kuzingatia ipasavyo miongozo yote inayotolewa na Wizara

ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Serikali kwa ujumla.

24. Mheshimiwa Spika, katika muktadha huu, Tanzania inaungana na Umoja wa Afrika, pamoja na viongozi mbalimbali wa nchi za Afrika kumwunga mkono Dkt. Tedros Adhanom Ghebreyesus, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa namna anavyoendelea kuliongoza vyema Shirika hili kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa COVID-19. Tunapenda kulitia moyo Shirika hilo chini ya uongozi mahiri wa Dr. Tedros kuendelea kufanya kazi kwa weledi ili kuiokoa dunia yetu dhidi ya magonjwa mbalimbali ikiwemo COVID-19. Tanzania inalishukuru Shirika hilo kwa miongozo na misaada linayotoa kwenye mapambano dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19. Kadhalika, tunawashukuru sana washirika wetu wote wa maendeleo kwa kuunga mkono jitihada za Serikali katika kupambana na ugonjwa huo hatari.

4.2 Hali ya siasa, ulinzi na usalama

25. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa fupi kuhusu hali ya Siasa, Ulinzi na Usalama wa dunia kama ifuatavyo:

Afrika

26. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuzipongeza nchi za Algeria, Botswana, Komoro, Namibia, Msumbiji, Mauritius, Togo na Tunisia, kwa kufanya chaguzi katika hali ya amani na utulivu katika kipindi cha mwaka 2019/2020. Hali hii, inaashiria kuimarika kwa misingi ya demokrasia na utawala bora katika Bara la Afrika. Aidha, pamoja na hali ya kisiasa kuwa ya kuridhisha, tishio la ugaidi, uwepo wa vikundi vya waasi, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, biashara ya dawa za kulevya na utakatishaji wa fedha haramu bado ni changamoto kwa nchi nyingi za Bara la Afrika na duniani kwa ujumla.

Algeria

27. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini Algeria imeimarika baada ya uchaguzi wa Rais uliofanyika mwezi Desemba 2019 na kumpata Rais mpya wa nchi hiyo Mheshimiwa Abdelmadjid Tebboune. Ni matumaini yetu kuwa, kuimarika kwa usalama wa nchi hiyo kutaendelea kuwa na mchango mkubwa katika kudumisha amani Barani Afrika.

Burundi

28. Mheshimiwa Spika, hali ya siasa, ulinzi na usalama nchini Burundi imeimarika hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Mei, 2020. Aidha, tunaupongeza uamuzi wa Mheshimiwa Pierre Nkurunziza, Rais wa Jamhuri ya Burundi kwa kutangaza kuondoka madarakani kwa amani baada ya kumaliza muda wake. Uamuzi huo wa kurithishana madaraka kwa njia ya amani ni ishara njema ya kuimarika kwa demokrasia nchini humo. Ni matumaini yetu kwamba Jumuiya ya Kimataifa itaiunga mkono Serikali mpya ya nchi hiyo ili iweze kutimiza matarajio ya Warundi katika harakati za maendeleo ya nchi hiyo na ya ukanda mzima wa Afrika Mashariki.

Cameroon

29. Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa nchini Cameroon ni tulivu ingawa imeendelea kukabiliwa na tofauti kati ya Majimbo yanayozungumza Kifaransa dhidi ya majimbo yanayozungumza Kiingereza. Majimbo yanayozungumza Kiingereza kwa muda mrefu yamekuwa yakidai kujitenga kutoka Cameroon inayoongozwa na jamii inayozungumza Kifaransa na kuunda Taifa lao la

Ambazonia. Sababu zinazochangia kuwepo madai hayo ni jamii hiyo inayozungumza Kiingereza kutoridhishwa na muundo wa utawala, kukosekana kwa usawa wa kisiasa, kiuchumi na kijamii na kutoridhishwa na uendeshaji wa chaguzi nchini humo kama ilivyodhihirika mwezi Februari, 2020 ambapo Cameroon ilifanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliosusiwa na Majimbo ya jamii inayozungumza Kiingereza chini ya Chama Kikuu cha Upinzani cha “Movement for Rebirth of Cameroon” kwamba haukuwa huru na wa haki.

30. *Mheshimiwa Spika*, hatua iliyochukuliwa na Serikali ni pamoja na kutoa hadhi maalum ya kiutawala kwa Majimbo hayo ya Kiingereza, kuitisha mijadala ya amani ya kitaifa pamoja na kuwaachia huru wafungwa wa kisiasa akiwemo Bw. Maurice Kamto, Kiongozi Mkuu wa upinzani. Tunazisihi pande zinazohasimiana kuendelea na majadiliano ili kumaliza tofauti zao kwa njia ya amani na hatimaye kupata suluhu ya kudumu.

Jamhuri ya Afrika ya Kati

31. *Mheshimiwa Spika*, hali ya kisiasa nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati inaendelea kuimarika kufuatia kusainiwa kwa Makubaliano ya Kisiasa

ya Amani na Maridhiano baina ya Serikali na vikundi vyenye silaha mwezi Februari 2019 kwa lengo la kusitisha mapigano. Hivi sasa nchi hiyo inaendelea na ujenzi wa taasisi za kisiasa na utendaji ili kukabiliana na changamoto za kusuasua kufikia malengo ya makubaliano. Aidha, nchi hiyo inatarajia kufanya uchaguzi mkuu kati ya mwaka 2020 na 2021. Ni matumaini yetu kuwa uchaguzi huo utafanyika katika mazingira huru na ya haki.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

32. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felix Antoine Tshisekedi Tshilombo, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) aliunda Baraza la Mawaziri mwezi Agosti 2019 lenye kujumuisha mawaziri kutoka chama cha upinzani cha *Common Front for Congo* (FCC) kinachoongozwa na Mheshimiwa Joseph Kabila aliyekuwa Rais wa nchi hiyo. Tangu aingie madarakani na kuunda Baraza la Mawaziri, Mheshimiwa Felix Tshisekedi ameendelea kujenga umoja wa kitaifa, kuimarisha amani na utulivu, kuhuisha taasisi za umma na kujenga mahusiano mema kwa majirani zake. Hata hivyo, hali ya usalama Mashariki mwa DRC haijatengamaa kutokana na kukabiliwa na mashambulizi kutoka kwa vikundi vya waasi

vyenye silaha. Serikali ya nchi hiyo kwa kushirikiana na vikosi vya Umoja wa Mataifa inaendelea na jitihada za kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo hilo.

33. Mheshimiwa Spika, tunatoa rai kwa Jumuiya ya Kimataifa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika juhudi za kurejesha amani jumuishi na ya kudumu nchini humo.

Kenya

34. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kidugu na wa kihistoria kati ya nchi yetu na nchi ya Kenya. Uhusiano huo mzuri umewezesha nchi zetu kuendelea kushirikiana katika masuala mbalimbali kama ilivyodhihirishwa na hatua ya Mhe. Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya ambapo tarehe 24 alimtuma Mjumbe wake Maalum, Mhe. Monica Kathina Juma, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, kwa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuja kukabidhi fedha kiasi cha Shilingi za Tanzania milioni 170, Shilingi za Kenya 171,000 na Dola za Marekani 77,500 zilizoibiwa mwaka 2004 katika Benki ya NBC,

Tawi la Moshi; pamoja na vipande vya dhahabu vyenye uzito wa kilo 35.267 vilivyokuwa vimetoroshwa kutoka hapa nchini mwaka 2018 na kukamatwa nchini Kenya.

35. Mheshimiwa Spika, kukabidhiwa kwa dhahabu na fedha hizo ni ishara ya uhusiano mzuri uliopo baina ya nchi hizi mbili na pia ni matokeo ya utekelezaji wa Sera yetu ya Mambo ya Nje katika kulinda maslahi ya nchi yetu.

36. Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Novemba, 2019, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alinituma kuwasilisha ujumbe wake maalum kwa Mhe. Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya. Nikiwa nchini humo, nilialikwa na Mhe. Rais Kenyatta kumwakilisha Mhe. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupewa fursa ya kuzungumza katika uzinduzi wa mpango wa amani na maridhiano ujulikanao kama *“Building Bridges Initiatives - BBI”* wenye lengo la kujenga umoja wa kitaifa kufuatia mpasuko wa kisiasa baada ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2017. Katika hotuba yangu, niliwaomba Wakenya kumaliza tofauti zilizopo na kuijenga Kenya yenye umoja na maelewano. Nitumie fursa

hii, kuwatakia kila la kheri wenzetu Wakenya katika kutekeleza mpango huo.

Komoro

37. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini Komoro kwa ujumla ni ya kuridhisha licha ya kuendelea kuwepo kwa changamoto za kisiasa. Msingi wa changamoto hizo ni madai ya vyama vya upinzani kwamba Uchaguzi Mkuu wa Rais uliofanyika tarehe 24 Machi, 2019 haukuwa huru na wa haki. Kutokana na madai hayo, vyama hivyo vilisusia Uchaguzi wa Wabunge na Magavana uliofanyika mwezi Februari, 2020.

38. Mheshimiwa Spika, madai mengine ya wapinzani ni kwamba Katiba ya nchi hiyo, iliyofanyiwa mabadiliko mwezi Julai 2018, haitoi mgawanyo sawa wa madaraka kwa visiwa vitatu vinavyounda Muungano wa Komoro, kinyume na Makubaliano ya Ugawaji wa Madaraka (Fomboni Agreement) ya mwaka 2002 ambayo yalileta amani, maelewano na muafaka wa kitaifa nchini humo. Tunatoa rai kwa pande zinazohasimiana kumaliza tofauti zao kwa njia ya mazungumzo ili kupata suluhu ya kudumu.

Somalia

39. Mheshimiwa Spika, nchi ya Somalia inaendelea kupiga hatua katika kuimarisha usalama ikiwa ni matokeo ya Serikali ya nchi hiyo kusimamia vyema vipaumbele vilivyoainishwa katika makubaliano ya amani na ukuaji wa uchumi. Pamoja na kupiga hatua katika utekelezaji wa makubaliano hayo, Somalia bado inaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwepo wa vikundi vya kigaidi ambavyo vinaendeleza mashambulizi yanayolenga kudhoofisha taasisi za umma, Misheni ya Afrika ya Kulinda Amani Somalia (AMISOM) na kuleta madhara kwa raia wasio na hatia. Tunatoa rai kwa Jumuiya ya Kimataifa na wapenda amani wote kushirikiana na Serikali ya Somalia katika kutatua changamoto za kiusalama zinazoikabili nchi hiyo.

Sudan

40. Mheshimiwa Spika, kufuatia kusainiwa kwa Makubaliano ya Kikatiba tarehe 17 Agosti, 2019 kati ya Baraza la Mpito la Jeshi la Sudan na Vyama vya Kiraia vya Kutetea Uhuru na Mabadiliko, hali ya amani nchini humo imeendelea kuimarika. Katika kutekeleza

makubaliano hayo, Serikali ya Mpito iliundwa kuliongoza Taifa hilo kwa kipindi cha miezi 39. Pamoja na kuundwa kwa Serikali ya Mpito changamoto za kiusalama zimeendelea kujitokeza. Mathalani, mwezi Machi 2020 Mheshimiwa Abdallah Hamdok, Waziri Mkuu wa nchi hiyo alinusurika katika jaribio la kuuawa. Tanzania inaungana na Jumuiya ya Kimataifa kulaani vikali jaribio hilo ovu.

Sudan Kusini

41. Mheshimiwa Spika, kufuatia makubaliano yaliyofanyika mwezi Februari 2020 ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa nchini Sudan Kusini, hali ya kisiasa na usalama imeanza kuimarika. Makubaliano hayo yanalenga kujenga umoja wa kitaifa baina ya jamii ndani ya nchi hiyo. Tunazisihi pande zote zinazohusika kuendelea kuheshimu na kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa.

Libya

42. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini Libya bado si nzuri kutokana na kuendelea kwa mapigano kati ya vikosi vya Serikali ya Mpito inayotambulika na Jumuiya ya Kimataifa na

vikundi vinavyoipinga Serikali. Tanzania inasikitishwa na hali hiyo na inaungana na Jumuiya ya Kimataifa kuzitaka pande hizo mbili kuheshimu Makubaliano ya kusitisha mapigano pamoja na Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa juu ya vikwazo vya silaha dhidi ya Libya. Hivyo, Tanzania inatoa wito kwa pande zinazohusika na mgogoro huo kurejea katika meza ya mazungumzo ili kutafuta suluhisho la kudumu kwa njia ya amani. Aidha, tunatoa rai kwa Jumuiya ya Kimataifa na wadau wa amani nchini Libya kushirikiana katika kumaliza changamoto za kiusalama zinazoikabili nchi hiyo.

Msumbiji

43. Mheshimiwa Spika, hali ya kisiasa nchini Msumbiji inaendelea kuimarika kufuatia kusainiwa kwa makubaliano ya amani baina ya Serikali na chama cha upinzani cha RENAMO mwezi Agosti, 2019. Makubaliano hayo yalifuatiwa na uchaguzi uliofanyika mwezi Oktoba 2019 ambapo chama cha RENAMO kilishiriki. Hata hivyo, Msumbiji imeendelea kukabiliwa na matukio ya mashambulizi ya kigaidi hususan katika Jimbo la Cabo Delgado lililopo kaskazini mwa nchi hiyo linalopakana na nchi yetu. Tanzania na Msumbiji

zinaendelea kushirikiana ili kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo la mpaka.

Guinea Bissau

44. Mheshimiwa Spika, hali ya usalama inaendelea kuimarika nchini Guinea Bissau baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika mwezi Desemba 2019 kuwa wa amani, huru na haki. Katika uchaguzi huo, chama cha MADEM – G15 kilichokuwa cha upinzani kilitangazwa kuwa mshindi ingawa matokeo ya uchaguzi huo yalipingwa na chama kilichokuwa madarakani cha PAIGC, hali iliyosababisha vurugu na kushindwa kubadilishana madaraka kwa njia ya amani. Ni matarajio yetu kuwa, pande zinazokinzana nchini humo zitarudi kwenye meza ya mazungumzo kwa lengo la kutafuta suluhu ya kudumu kwa manufaa ya Taifa hilo.

Ulaya na Amerika

45. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya siasa, ulinzi na usalama katika nchi za Ulaya na Amerika imeendelea kuimarika. Pamoja na kuimarika kwa hali hiyo, eneo hilo limeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

Venezuela

46. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, nchi ya Venezuela imeendelea kukabiliwa na mgogoro wa kisiasa unaotokana na maandamano ya kupinga Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Nicolas Maduro, Rais wa Venezuela. Mgogoro huo, uliibuka baada ya kambi ya upinzani kupinga matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2018 yaliyomweka madarakani Rais Nicolas Maduro kwa madai kuwa hayakuwa halali.

47. Mheshimiwa Spika, kudumu kwa muda mrefu kwa mgogoro huo kumeleta athari kubwa za kiuchumi na kijamii katika nchi hiyo. Tunatoa rai kwa pande zinazohasimiana kukaa kwenye meza ya mazungumzo kwa ajili ya kupata suluhisho la kudumu kwa maendeleo na ustawi wa watu wa Venezuela.

Umoja wa Ulaya

48. Mheshimiwa Spika, Bara la Ulaya limeshuhudia matukio machache yenye viashiria vya ugaidi ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Baadhi ya matukio ya kigaidi yaliyoripotiwa katika kipindi hiki ni pamoja na yale yaliyotokea katika

miji ya Milan, Italia na Hanau, Ujerumani. Aidha, kufuatia hatua ya Uturuki kufungua mipaka yake, eneo la Umoja wa Ulaya linakabiliwa na ongezeko kubwa la wakimbizi kutoka Syria na nchi nyingine za Mashariki ya Kati na zinazokabiliwa na migogoro ya kivita na wahamiaji kutoka bara la Afrika. Hali hii, imeleta taharuki miongoni mwa viongozi na wananchi katika Umoja huo.

Uingereza

49. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2020 nchi ya Uingereza ilijitoa katika Umoja wa Ulaya (Brexit). Mchakato wa kujitoa ulianza tangu mwezi Juni 2016, baada ya wananchi wa nchi hiyo kupiga kura ya kujiondoa kwenye Umoja huo. Kufuatia matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Desemba 2019 na kukipa ushindi Chama cha Wahafidhina (Conservatives), suala ambalo lilitoa mamlaka zaidi kwenye mchakato wa Brexit, kwa sasa, nchi hiyo inaendelea kujadiliana na Umoja wa Ulaya ili kufikia makubaliano ya ushirikiano baada ya kujiondoa rasmi katika Umoja huo ifikapo mwezi Desemba 2020.

50. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Uingereza na Umoja wa Ulaya wote ni miongoni mwa washirika muhimu wa Tanzania katika

maendeleo, biashara na uwekezaji, Wizara inaendelea kufuatilia kwa karibu majadiliano hayo.

Ubelgiji

51. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2020, Ubelgiji ilifanikiwa kuunda Serikali ya Shirikisho kufuatia uchaguzi uliofanyika mwezi Mei 2019. Serikali hiyo inayoundwa na mseto wa vyama vya wachache (Reformist Movement (MR), Christian Democratic and Flemish (CD&V), Open Flemish Liberals and Democrats (Open VLD) inaongozwa na Mhe. Sophie Wilemés ambaye anakuwa mwanamke wa kwanza kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo. Tofauti na chaguzi zingine zilizopita, katika uchaguzi huo, vyama vya mreno wa kushoto vimepata uungwaji mkono zaidi, hali iliyosababisha kuwepo na ugumu zaidi katika kufikia makubaliano ya kuunda Serikali ya shirikisho kutokana na kuwepo na tofauti kubwa za kimitzamo na kiitikadi. Huu ni mwendelezo wa vuguvugu la vyama vyenye misimamo mikali kuendelea kuungwa mkono katika chaguzi zilizofanyika katika nchi mbalimbali za Ulaya katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni.

Ufaransa

52. Mheshimiwa Spika, mwaka 2019, Ufaransa ilishuhudia maandamano makubwa yajulikanayo kama *yellow vests* kupinga uamuzi wa kufanya mabadiliko/mageuzi katika Mfuko wa Hazina wa Pensheni ya Uzeeni kwa wafanyakazi, kuongezeka kwa bei ya dizeli, kupanda kwa gharama za maisha na mabadiliko ya kodi yasiyokuwa na uwiano. Mageuzi hayo ni mojawapo kati ya mambo ambayo Mhe. Emmanuel Macron, Rais wa Jamhuri ya Ufaransa aliahidi kutekeleza katika kipindi cha uongozi wake. Kwa wafanyakazi wengi, mabadiliko haya yameonekana kuwa ya kinyanyasaji na yasiyo na usawa kwa kuwa yatawachelewesha kustaafu kinyume na umri uliowekwa kisheria wa miaka 62 au malipo yao ya uzeeni kupunguzwa.

53. Mheshimiwa Spika, maandamano hayo yalipelekea shughuli nyingi nchini humo kusimama ikiwemo huduma za kijamii, usafiri wa umma ambapo asilimia 90 ya safari za treni za mwendokasi na zile za kawaida zilifutwa. Vilevile, kwa upande wa usafiri wa anga maandamano hayo yalipelekea kampuni nyingi za ndege za nchini humo kufuta asilimia 30 ya safari zake za

ndani na zile za kimataifa.

54. Mheshimiwa Spika, kwa sasa maandamano nchini Ufaransa yametulia na mpango wa kubadilisha Mfuko wa Hazina wa Pensheni ya Uzeeni kwa wafanyakazi umepelekwa Bungeni kama Muswada kwa ajili ya kufanyiwa mapitio na baadaye kupitishwa na Wabunge ili kuanza utekelezaji wake.

Asia na Australasia

China

55. Mheshimiwa Spika, dunia ilishuhudia machafuko na ghasia katika eneo la Hong Kong yaliyoanza mwezi Juni 2019 na kudumu takriban kwa miezi sita ambapo chanzo chake kilikuwa kulalamikiwa kwa muswada wa sheria ya kutaka wahalifu wa kisiwa cha Hong Kong wapelekwe kushtakiwa upande wa China Bara. Hata hivyo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali Kuu ya China ilifanikiwa kusitisha machafuko hayo kwa njia ya mazungumzo baina ya Serikali Kuu ya China na Serikali ya Eneo Maalum la Kiutawala la Hong Kong ambapo viongozi wa pande zote mbili walikubaliana

kuendelea kuitambua Sera ya China Moja, Mifumo Miwili (One China, Two Systems).

56. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine iliyochukuliwa ni kwa Serikali Kuu ya China kumteua kada wake wa ngazi za juu wa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) kuwa Mkuu wa Ofisi ya Uhusiano kati ya Serikali Kuu ya China na Serikali ya Eneo Maalum la Kiutawala la Hong Kong. Ni dhahiri kuwa uteuzi huo utasaidia kuimarisha uhusiano mzuri uliopo sambamba na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Jamhuri ya Korea

57. Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Korea ilifanya Uchaguzi Mkuu wa Wabunge tarehe 19 Aprili 2020. Kwa mujibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Korea, Chama tawala cha Korea, *Democratic Party of Korea* kilishinda uchaguzi huo kwa kishindo kwa kupata viti 180 sawa na asilimia 60 ya viti vyote 300 vilivyokuwa vinashindaniwa. Ushindi huo ni mkubwa kwa Chama tawala tangu kuanzishwa kwa mfumo wa demokrasia huru katika uchaguzi wa mwaka 1987 na imedhihirisha ukomavu wa demokrasia nchini humo.

58. Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, Jamhuri ya Korea ilifanya uchaguzi huo katika kipindi kigumu ambacho dunia ikiwa inaandamwa na janga la homa kali ya mapafu inayosababishwa na Virusi vya Corona (Covid-19). Kwa muktadha huo, Serikali ya Tanzania inaipongeza Jamhuri ya Korea kwa kufanikisha Uchaguzi Mkuu pamoja na changamoto ya uwepo wa ugonjwa huo.

Japan na Jamhuri ya Korea

59. Mheshimiwa Spika, mgogoro wa kisiasa kati ya Japan na Jamhuri ya Korea bado umeendelea kuwa changamoto. Hali hii imetokana na Japan kuiondoa Korea katika nchi za kipaumbele kwenye masuala ya kibiashara hususan ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Hatua hii imefikiwa na Japan baada ya mwaka 2019 Korea kuibua tena madai ya kulipwa fidia kutokana na vitendo vinavyodaiwa kuwa vya unyanyasaji ambavyo wananchi wake walipata wakati nchi hiyo ikitawaliwa na Japan.

60. Mheshimiwa Spika, athari ya mgogoro huo siyo tu kwa nchi hizo mbili bali pia kwa nchi mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania kutokana

na ukweli kwamba nchi hizo ni miongoni mwa wazalishaji na wauzaji wakubwa wa bidhaa za viwandani zikiwemo za TEHAMA ambazo Tanzania ni mnufaika. Aidha, Tanzania inaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na viongozi wa mataifa hayo katika kutatua mgogoro huo kwa njia ya mazungumzo ya kidiplomasia.

Mashariki ya Kati

61. *Mheshimiwa Spika*, baadhi ya nchi za Mashariki ya Kati zimeendelea kukabiliwa na machafuko ya kisiasa na vita vya wenyewe kwa wenyewe yanayotishia hali ya usalama katika eneo lote la ukanda huo na duniani kwa ujumla. Nchi za Syria, Yemen na Iraq ndizo zilizoathiriwa zaidi na machafuko hayo. Hali hiyo, imesababisha silaha kuzagaa kiholela, kuwepo kwa vikundi vya kigaidi, uharamia na uhalifu mwingine. Aidha, machafuko hayo yamesababisha kuongezeka kwa idadi ya wakimbizi katika mataifa mbalimbali duniani kutoka nchi hizo. Katika kipindi hiki, kumetokea maandamano katika nchi za Iraq na Lebanon, kutokana na wananchi kudai kuwepo kwa hali mbaya ya kiuchumi. Maandamano hayo, yamesababisha kujiuzulu kwa Mheshimiwa Saad Hariri, Waziri Mkuu wa Lebanon na Mheshimiwa Adel Abdul Mahdi, Waziri Mkuu wa Iraq.

62. Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuimarisha ushirikiano na nchi za Mashariki ya Kati, ambalo ni eneo la kimkakati katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Pamoja na changamoto za kisiasa na kiusalama zilizopo katika eneo hilo zipo fursa nyingi za kiuchumi ambazo tunanufaika nazo. Mathalan, kupitia balozi zetu katika miji ya Doha, Tel Aviv, Muscat, Riyadh, Kuwait na Abu Dhabi tumeendelea kuhakikisha Taifa linanufaika na fursa za uwekezaji na biashara zinazotokana na kuimarika kwa uchumi wa eneo hilo hususan nchi za ghuba.

63. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki ambacho uchumi wa dunia unatabiriwa kudorora, ni ukweli usioplingika kuwa nchi za Mashariki ya Kati zenye uchumi uliojengwa kwa mipango thabiti katika sekta ya nishati ya mafuta na gesi asilia zitaendelea kuwa mshirika muhimu na kimkakati kwa Tanzania.

64. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kutumia fursa zinazotokana na ushirikiano na nchi za ukanda huo, Wizara itaendelea kuimarisha mawasiliano yatakayoweza upatikanaji wa masoko ya

bidhaa zinazozalishwa nchini, kuhamasisha utalii na kuvutia uwekezaji nchini.

65. Mheshimiwa Spika, aidha, tutaendelea kuimarisha ushirikiano na mifuko ya fedha pamoja na taasisi za misaada ikiwemo Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*Kuwait Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (*Saud Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi (*Abu Dhabi Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Khalifa (*Khalifa Fund*), Benki ya Nchi za Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta (*OFID*) kwa ajili ya kupata mikopo ya masharti nafuu na misaada ya kuboresha huduma za jamii nchini.

66. Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara imekuwa ikifuatilia kwa karibu na kuchambua hali ya siasa na usalama katika nchi mbalimbali za Mashariki ya Kati na kutoa ushauri kuhusu namna ya kuboresha mahusiano na nchi hizo utakaosaidia kuleta amani ya kudumu kwa maslahi ya kiuchumi kwa Taifa katika eneo hilo. Sehemu ya juhudi zinazofanyika ni pamoja na kushiriki katika mijadala na kuunga mkono maazimio mbalimbali ya jumuiya ya kimataifa yanayolenga kumaliza migogoro kwa njia za kidiplomasia katika nchi za eneo hilo.

Mpango wa Amani wa Israel na Palestina

67. Mheshimiwa Spika, mwezi Januari 2020 Serikali ya Marekani ilitangaza mpango mpya wa Amani wa Mashariki ya Kati unaohusu Palestina na Israel kupata suluhisho la kuwa nchi mbili zinazokaa kwa amani. Mpango huo haujaungwa mkono na Palestina na Jumuiya ya nchi za Kiarabu.

68. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kueleza msimamo wa Tanzania katika mgogoro wa Israel na Palestina kuwa nchi yetu itaendelea kuzingatia misingi tuliyoachiwa na waasisi wa Taifa letu ambayo ndiyo nguzo ya Sera yetu ya Mambo ya Nje ya kupigania haki ya kujitawala wenyewe, kuheshimu mipaka ya nchi na kuunga mkono maazimio ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kuhusiana na mgogoro huo. Hivyo, Tanzania itaendelea kuzishauri pande zote husika, kuheshimu makubaliano yaliyofikiwa kwa pamoja. Tanzania inaamini suluhisho la kudumu katika mgogoro huo ni la kuwa na nchi mbili ambazo zitakaa kwa pamoja ikiwa ni Israel salama na Palestina huru.

Mgogoro katika Nchi za Ghuba

69. *Mheshimiwa Spika*, mahusiano katika nchi za Ghuba yameendelea kuimarika. Hivi karibuni kati ya mwezi Novemba 2019 na mwezi Januari 2020 yalifanyika mazungumzo baina ya nchi ya Qatar na nchi zilizoikea vikwazo ikiwemo Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu, Bahrain, Misri na Sudan. Ni matumaini yetu kuwa mazungumzo hayo yataendelea kwa lengo la kumaliza tofauti zilizojitokeza baina ya nchi hizo.

5.0 NAFASI YA TANZANIA KIMATAIFA NA KIKANDA

70. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania ikiwa Nchi Mwanachama wa Umoja wa Mataifa imeendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za Umoja wa Mataifa, Taasisi na Mashirika yake na pia katika mikutano, mijadala na shughuli mbalimbali za Umoja huo. Miongoni mwa mijadala hiyo ilifanyika kwenye Kikao cha 74 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambapo nilimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kikao hicho nilitoa hotuba iliyoelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano kwenye sekta za afya; elimu; maji; usafiri wa anga; nishati na ujenzi.

Aidha, hotuba hiyo ilieleza utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama vile ujenzi wa reli ya kisasa; bwawa la ufuaji umeme la Mwalimu Nyerere; ufufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania; ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege; na usambazaji wa umeme vijijini. Vilevile, nilieleza mafanikio ya Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na kukuza demokrasia nchini.

71. Mheshimiwa Spika, katika hotuba hiyo nilieleza pia msimamo wa Tanzania katika kupinga vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Zimbabwe pamoja na vipaumbele vyetu katika nafasi ya Uenyekiti wa SADC kwa mwaka 2019/2020. Aidha, Tanzania ilizisihi Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa kushirikiana kiuchumi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo baada ya hali ya amani nchini humo kuanza kuimarika.

72. Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kutekeleza majukumu yake kimataifa kwa mujibu wa mikataba na makubaliano mbalimbali tuliyosaini na kuridhia, ikiwemo Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063 iliyopitishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mwaka 2015 na Ajenda ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 iliyopitishwa na Umoja wa Mataifa

mwaka 2015. Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imewianisha mikakati ya maendeleo iliyopo kwenye ajenda hizo na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021.

73. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango huu, umeleta manufaa makubwa katika kujenga Tanzania ya uchumi wa viwanda na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Julai 2019, Tanzania iliwasilisha taarifa yake ya hiari kwenye Umoja wa Mataifa kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (Voluntary National Review 2019) yanayoenda sanjari na utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

74. Mheshimiwa Spika, Tanzania pia imeendelea kupokea na kuhifadhi wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi mbalimbali duniani ikiwa ni pamoja na Burundi. Kufuatia kuimarika kwa hali ya amani nchini Burundi, Tanzania kwa kushirikiana kwa karibu na wadau wote wanaohusika ikiwemo Serikali ya Burundi, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi na

Shirika la Kimataifa la Wahamaji, imeendelea na zoezi la kuwarejesha kwa hiari wakimbizi wa Burundi nchini mwao. Zoezi hili linatekelezwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zote za kitaifa na kimataifa.

75. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Jumuiya ya Kimataifa kwa kuunga mkono utekelezaji wa zoezi hili. Aidha, nitumie fursa hii kuzisihi nchi na taasisi zisizo za kiserikali kuacha mara moja hujuma na propaganda za kukwamisha zoezi hili. Tanzania inaamini wakimbizi wa Burundi waliopo hapa nchini wakirejea nchini mwao watakuwa na mchango mkubwa katika ujenzi na ustawi wa Taifa lao.

76. Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kushughulikia changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yanahatarisha maisha, ustawi na maendeleo ya nchi zetu. Aidha, nchi mbalimbali zimeendelea kukabiliana na majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi. Mathalan, katika kipindi hiki, baadhi ya nchi za SADC, zikiwemo Komoro, Malawi, Msumbiji, Madagascar na Zimbabwe zilikabiliwa na majanga ya asili ikiwemo mafuriko na ukame uliosababisha

kuwepo kwa upungufu wa chakula katika nchi hizo.

77. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pole kwa nchi zote zilizopata majanga hayo ambayo yanatukumbusha umuhimu wa Jumuiya ya Kimataifa kushirikiana katika kuzuia athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi. Natoa rai kwa mataifa yote duniani kushirikiana katika kuzuia na kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kutekeleza Mikataba mbalimbali ya kimataifa, ukiwemo Mkataba wa Paris wa mwaka 2015.

78. Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kulipa umuhimu mkubwa suala la amani na usalama duniani ambalo ni miongoni mwa tunu za Taifa letu tangu kupata uhuru. Ili kuenzi tunu hizi na kutambua umuhimu wa kulinda na kudumisha amani na usalama duniani, nchi yetu imeendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika ulinzi wa amani duniani. Katika kutekeleza hilo, hadi sasa nchi yetu imepeleka walinda amani 2,303 kwenye misheni za kulinda amani za Umoja wa Mataifa zilizopo katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Lebanon, Darfur - Sudan, Sudan Kusini na Jimbo la Abyei.

79. Mheshimiwa Spika, kwa nafasi yetu ya uenyekiti wa SADC tutaendelea kushirikiana na mataifa mengine kushughulikia masuala ya amani na usalama katika Bara letu la Afrika, hususan hali ya usalama nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Lesotho. Nitumie fursa hii kuisihi Jumuiya ya Kimataifa kuendelea kuunga mkono jitahada za kudumisha amani katika nchi hizo na maeneo mengine duniani.

80. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika shughuli mbalimbali za Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibeani na Pasifiki (OACPS), ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maamuzi kupitia mikutano mbalimbali. Katika kutekeleza azma hii, niliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika mwezi Desemba 2019 jijini Nairobi, Kenya nikimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

81. Mheshimiwa Spika, kupitia Mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kujumuisha zao la korosho kwenye orodha ya mazao ya kimkakati ndani ya OACPS ambayo yatanufaika na Programu ya Mnyororo wa Thamani wa OACPS. Programu hii, iliyotengewa kiasi cha Euro milioni 140 itatoa

fursa kwa wakulima kupata mikopo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji, kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

6.0 KUJENGA NA KULINDA TASWIRA YA NCHI KIMATAIFA

82. *Mheshimiwa Spika*, hivi karibuni kumekuwa na tuhuma dhidi ya Tanzania kutoka kwa baadhi ya nchi, taasisi za kimataifa na taasisi zisizo za kiserikali kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwemo haki ya kujieleza na kutoa maoni pamoja na haki ya kujumuika na kukusanyika. Tuhuma hizo zinahusishwa na marekebisho ya baadhi ya sheria zetu ambazo ni: Sheria ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016; Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya Mwaka 2018; Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 2018; Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2018; na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2019.

83. *Mheshimiwa Spika*, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tuhuma hizo hazina ukweli wowote na zina nia oву za kuibagaza nchi yetu kwa kuwa imepiga hatua kubwa katika kujiletea maendeleo kwenye nyanja mbalimbali. Tuhuma zinazotolewa hutokana na uwepo wa

tofauti za kimtazamo baina yetu na nchi au taasisi zinazotoa tuhuma hizo.

84. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutumia majukwaa mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu kutoa ufafanuzi kuhusu tuhuma hizo kwa sababu uwongo na upotoshaji hautakiwi kukaliwa kimya. Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua na kuheshimu, wajibu wake Kikatiba na Mikataba ya Kimataifa ya kulinda na kudumisha haki zote za binadamu ikiwemo za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni zote zikiwa na umuhimu ulio sawa kwa ustawi na maendeleo ya Watanzania.

85. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali kuufahamisha ulimwengu namna inavyotetea na kusimamia haki za binadamu hapa nchini, mwezi Februari 2020, niliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Kikao cha 43 cha Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu. Kwenye Kikao hicho nilieleza kuhusu mafanikio ya Serikali katika kulinda na kusimamia haki za elimu, afya, upatikanaji wa maji safi na salama, umeme na

maendeleo ya kiuchumi. Aidha, nilielezea mafanikio yaliyopatikana katika kuongeza uwajibikaji kwa watumishi na viongozi wa umma; kupambana na vitendo vya rushwa; vita dhidi ya biashara ya dawa za kulevya; kuongezeka kwa kiwango cha ukusanyaji kodi; na kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ili kuwahudumia wananchi wetu ipasavyo.

86. Mheshimiwa Spika, kufuatia ufafanuzi wa mara kwa mara kuhusu tuhuma hizo kwenye Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, Jumuiya ya Kimataifa imeanza kutambua mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kulinda na kusimamia haki za binadamu. Kwa mfano, kwenye Kikao cha 43, cha Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, Bi. Michelle Bachelet, Kamishna wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa, aliipongeza Serikali ya Tanzania katika mapambano dhidi ya rushwa, kupunguza umaskini, kuimarisha miundombinu na kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa umma. Vilevile, Tanzania ilitajwa kwenye taarifa ya Mpango wa *Africa Landscape Restoration Initiative* kuwa ni miongoni mwa nchi chache duniani zinazotambua haki ya maji na mazingira safi kwa wananchi wake.

87. Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na mikakati mbalimbali iliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kulinda haki za watu wenye ulemavu wa ngozi, sasa Tanzania inatambulika kimataifa katika kulinda na kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Hatua hii, imedhihirika baada ya Tanzania kupongezwa katika taarifa ya Umoja wa Mataifa inayohusu haki za watu wenye ulemavu wa ngozi iliyowasilishwa mbele ya Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu mwezi Februari 2020.

88. Mheshimiwa Spika, Tanzania inatambua umuhimu wa uhuru wa vyombo vya habari na kuheshimu mchango wa vyombo hivyo katika kuchagiza maendeleo. Kwa umuhimu huo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa takwimu zilizopo, nchi yetu ina jumla ya vituo vya redio 152 ambapo vituo vitatu tu ndivyo vinavyomilikiwa na Serikali. Aidha, vituo vya televisheni vipo 34 na ni vituo viwili tu ndivyo vinamilikiwa na Serikali. Vilevile, kwa upande wa magazeti Serikali imetoa jumla ya leseni 172 ambapo asilimia 90 ya leseni hizo zimetolewa kwa sekta binafsi. Kwa kuzingatia takwimu hizi, ni

wazi kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika suala la uhuru wa vyombo vya habari.

89. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2020 Tanzania inatarajia kufanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani ambapo Watanzania wenye sifa watapata haki yao ya msingi ya Kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa. Hii ni moja ya nguzo kuu ya demokrasia tuliyojiwekea tangu tulipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi.

90. Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba niithibitishie Jumuiya ya Kimataifa kuwa Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 unafanyika katika mazingira ya uwazi, amani, uhuru na haki. Kama ilivyo kawaida yetu, wakati ukifika, tutazialika nchi na taasisi mbalimbali za Kimataifa kuja kuangalia uchaguzi wetu ili kujionea jinsi nchi yetu ilivyokomaa kidemokrasia na kuwa ni mfano wa kuigwa Barani Afrika na duniani kwa ujumla. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi Mahiri wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli umefanya mambo makubwa, mazuri na ya kihistoria kwa nchi na kwa Watanzania, ni dhahiri kuwa uchaguzi huu utakuwa ni wa kihistoria.

7.0 WATANZANIA KWENYE NAFASI ZA KIMATAIFA

91. Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, Watanzania wameendelea kuheshimika na kuaminika kwenye duru za kimataifa. Kwenye ngwe hii ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Tano tumeshuhudia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiteuliwa kuwa mmoja wa wajumbe wa Jopo la Ngazi za Juu la kumshauri Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu masuala ya Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi; na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa kuwa mwakilishi wa Umoja wa Afrika kwenye utatuzi wa mgogoro wa Libya.

92. Mheshimiwa Spika, kadhalika, Dkt. Stergomena Lawrence Tax alichaguliwa kuwa Katibu Mtendaji wa SADC kwa awamu ya pili mfululizo; na Dkt. Agnes Kijazi, Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania alichaguliwa kuwa Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani. Aidha, Bw. Gabriel Rugalema ameteuliwa kuwa Mwakilishi Mkazi wa Shirika la

Chakula na Kilimo Duniani (FAO) katika nchi ya Sierra Leone.

93. Mheshimiwa Spika, wengine ni Balozi Profesa Kennedy Gaston, ambaye alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Mashauriano ya Masuala ya Kisheria katika nchi za Asia na Afrika; Bw. Donatius Kamamba, alichaguliwa kuwa Mjumbe kwenye Kamati ya Urithi wa Dunia ya Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Mhandisi Steven Mlote aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Mheshimiwa Jaji Sauda Mjasiri aliyeteuliwa kuwa Jaji katika Mahakama ya Afrika Mashariki.

94. Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Stephen Masele (Mb) alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika; Mheshimiwa Jaji Iman Aboud alichaguliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Umoja wa Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; Dkt. Nyamajeje Wegoro aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Kanda ya Afrika Mashariki; Bi. Donatha Rugarabamu, Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP); Balozi Ali Mchumo aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la

Kimataifa linalosimamia mianzi; Mhe. Mboni Mhita (Mb), alichaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Vijana la Afrika; Bi. Maryam Salim Ahmed Salim aliyeteuliwa kuwa Meneja Mkazi wa Benki ya Dunia nchini Albania; Bi. Joyce Msuya aliyeteuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mpango wa Mazingira Duniani (UNEP); na Bi. Sabina Seja aliyeteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya kupambana na Rushwa ya Afrika.

95. Mheshimiwa Spika, hawa ni baadhi tu nilioweza kuwataja, hapana shaka kuna Watanzania wengi ambao wanashika nafasi za juu kwenye Mashirika na Taasisi mbalimbali za kimataifa. Tunawapongeza sana wote na tunajivunia.

96. Mheshimiwa Spika, Watanzania wameendelea kuheshimika siyo tu na Mashirika na Taasisi za Kimataifa bali pia na nchi moja moja. Mathalani, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu zoezi la mapokezi ya nishani ya juu ya urafiki ya Jamhuri ya Watu wa China iliyotolewa na Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China kwa Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni ishara ya kutambua na kuenzi mchango wake katika

kukuza urafiki kati ya China na Tanzania na Bara la Afrika kwa ujumla.

97. Mheshimiwa Spika, nishani hiyo hutolewa kwa watu mashuhuri waliotoa mchango mkubwa kwa Taifa la Watu wa China. Mheshimiwa Dkt. Salim anakuwa Mwafrika wa kwanza kupata Nishani ya Juu ya Urafiki ya Taifa la China kutokana na mchango wake alipokuwa Balozi na Mwakilishi wa Kudumu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa uliochangia kuiwezesha Jamhuri ya Watu wa China kuwa Mwanachama wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mwaka 1971. Aidha, Serikali ya China ilieleza kuwa Mheshimiwa Dkt. Salim alitoa mchango mkubwa katika kuimarisha uhusiano kati ya China na Tanzania wakati akishikilia nyadhifa mbalimbali za Kimataifa ikiwa ni pamoja na nafasi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika.

98. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim siyo tu kwa kupokea nishani hiyo bali pia kwa kuendelea kulijengea Taifa letu heshima kubwa kimataifa.

8.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020

99. Mheshimiwa Spika, katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2019/2020, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 166,926,820,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 162,926,820,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 4,000,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 152,717,723,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 10,209,097,000** ni kwa ajili ya Mishahara.

100. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Wizara ilikuwa imepokea kutoka HAZINA kiasi cha **Shilingi 133,300,900,671.84**. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na **asilimia 79.8** ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 124,186,236,675.44** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 8,626,758,000.00** kwa ajili ya mishahara. Aidha, katika kipindi hicho Wizara imepokea fedha za bajeti ya miradi ya maendeleo kiasi cha **Shilingi 487,905,996.40** kwa ajili ya miradi ya ukarabati wa nyumba ya makazi

ya Balozi wa Tanzania Ottawa na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Chuo cha Diplomasia.

101. Mheshimiwa Spika, katika fedha zilizotolewa, Wizara imetumia kiasi cha Shilingi **99,324,222,786.14**. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na **asilimia 75** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **91,390,079,647.28** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **7,596,237,142.46** kwa ajili ya mishahara. Aidha, Wizara imetumia kiasi cha Shilingi **337,905,996.40** kwa ajili ya mradi wa maendeleo wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Chuo cha Diplomasia.

102. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ilipanga kukusanya **Shilingi 2,550,879,072**. Kati ya kiasi hicho **Shilingi 67,980,000.00** ni maduhuli ya Makao Makuu ya Wizara na **Shilingi 2,482,899,072** ni maduhuli kutoka Balozi za Tanzania nje ya nchi. Vyanzo vya mapato hayo ni pamoja na uhakiki wa nyaraka, pango la majengo ya Serikali nje ya nchi na mauzo ya nyaraka za zabuni.

103. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2019 hadi tarehe 30 Aprili, 2020 Wizara

imekusanya jumla ya Shilingi **5,253,091,650.07** sawa na asilimia **206** ya lengo lililopangwa kwa mwaka 2019/2020. Ongezeko la maduhuli limetokana na baadhi ya balozi kuendelea kukusanya maduhuli ya viza kupitia utaratibu wa kawaida kabla ya kuanza kwa utaratibu wa kielektroniki (*e-visa*). Aidha, kuanzia mwezi Novemba 2019, Wizara inaendelea kukusanya maduhuli ya visa kwa njia ya kielektroniki baada ya Balozi kufungiwa mtandao huo.

104. *Mheshimiwa Spika*, baada ya kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi hicho.

105. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa majukumu ya Wizara unaongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015 - 2020; Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21); Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063; Ajenda ya mwaka 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; Mkakati wa Maendeleo

wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2017/2018 - 2021/2022; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Itifaki zake pamoja na Mikataba mingine ya Kikanda na Kimataifa; Mpango wa Maendeleo wa SADC uliofanyiwa maboresho wa mwaka 2015 – 2020; Mpango Mkakati wa Pili wa Asasi ya Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa mwaka 2016 – 2020; maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2019/2020; Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 – 2021/2022 na Maagizo mbalimbali yaliyotolewa kwa nyakati tofauti kwa Wizara na Viongozi wa Kitaifa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

106. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia miongozo hiyo, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

8.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje

8.1.1 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Afrika

Afrika Kusini

107. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Cyril Matamela Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini iliyofanyika mwezi Agosti 2019. Tanzania na Afrika Kusini zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya biashara na uwekezaji pamoja na kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kufuatia makubaliano hayo, mwezi Septemba 2019 Serikali ya Afrika Kusini ilitangaza kuanza rasmi kufundisha lugha ya Kiswahili kuanzia mwaka 2020. Wizara inaendelea kuratibu suala hili kwa kushirikiana na wadau wa kisekta.

Uganda

108. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na mahusiano mazuri na ya kidugu kati ya nchi yetu na Uganda, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda hapa

nchini. Wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais Museveni na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walizindua Jengo la Taasisi ya Mwalimu Nyerere lililopo jijini Dar es Salaam. Viongozi hao pia, walishiriki katika Kongamano la Biashara kati ya nchi hizi mbili lililofanyika kwa lengo la kutangaza fursa za biashara na uwekezaji. Fursa hizo, ni pamoja na huduma za uchukuzi zinazotolewa na Shirika la Ndege la Tanzania, Shirika la Reli Tanzania, Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania na Mamlaka ya Bandari Tanzania.

109. Mheshimiwa Spika, vilevile, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu ziara ya wataalam kutoka sekta ya uchukuzi kwa lengo la kutangaza na kuhamasisha matumizi ya Ushoroba wa Kati kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwa njia ya reli na kutoka Mwanza hadi Bandari ya Portbell, Uganda kwa njia ya maji kupitia Ziwa Victoria. Ziara hiyo ilitoa fursa kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Shirika la Reli Tanzania na Kampuni ya Huduma za Meli kujitangaza kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi hususan Uganda kutumia ushoroba huo kusafirisha mizigo yao.

110. *Mheshimiwa Spika*, katika ziara hiyo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) lilikubali kuendelea kutumia ushoroba huo kusafirisha chakula cha msaada kwenda kambi za wakimbizi zilizopo katika nchi za Uganda na Sudan Kusini.

Misri

111. *Mheshimiwa Spika*, katika kuenzi mahusiano ya kihistoria kati ya Tanzania na Misri, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Misri. Akiwa nchini Misri, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya mazungumzo rasmi na Mheshimiwa Dkt. Mostafa Madbouly, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipata nafasi ya kufanya mkutano na wafanyabiashara wa Misri na Watanzania wanaoishi nchini humo. Kutokana na ziara hiyo, Tanzania na Misri zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta za nishati; kilimo; mifugo na uvuvi; afya; biashara na uwekezaji; ulinzi na usalama; ujenzi, uchukuzi na mawasiliano.

Rwanda

112. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda kwa ajili ya kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa Rwanda. Ushiriki wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye maadhimisho hayo ni ishara ya uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na Rwanda pamoja na desturi ya Tanzania katika kudumisha ujirani mwema.

Burundi

113. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye ziara ya Mawaziri watatu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Burundi iliyofanyika nchini kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika sekta ya uchukuzi. Ujumbe huo ukiwa nchini, ulitembelea Bandari ya Dar es Salaam; Bandari Kavu ya kisasa inayojengwa eneo la Kwala mkoani Pwani na Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa. Kufuatia ziara hiyo, mwezi Agosti 2019, Serikali za Tanzania na Burundi zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya Uvinza – Msongati - Gitega. Ziara hiyo

ilihamasisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kujiunga kwenye mradi huo ili ufike katika maeneo ya Uvira na Kindu nchini DRC. Maandalizi ya utekelezaji wa Mradi huo ikiwemo upembuzi yakinifu yameanza.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)

114. *Mheshimiwa Spika*, katika kutumia fursa zilizopo katika maeneo ya kimkakati ikiwemo eneo la Mashariki mwa DRC, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kuwezesha majadiliano kati ya maafisa waandamizi wa Benki ya CRDB PLC ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Majadiliano hayo, yalilenga kuiwezesha benki ya CRDB kuanzisha shughuli za kibenki hususan katika eneo la Lubumbashi, mashariki mwa nchi hiyo. Hatua ya benki hiyo kuanzisha huduma zake nchini DRC itachochea kukua kwa wigo wa biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na DRC kwa kurahisisha miamala ya kibenki kwa wafanyabiashara.

8.1.2 Ushirikiano kati ya Tanzania na Nchi za Asia na Australasia

Viet Nam

115. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Trinh Dinh Dung, Naibu Waziri Mkuu wa Viet Nam ambaye aliambatana na ujumbe wa wafanyabiashara. Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Trinh na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walifanya mazungumzo na kukubaliana kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia ikiwemo Tanzania kufungua Ubalozi nchini Viet Nam na kuanzisha Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano. Mafanikio mengine yaliyopatikana wakati wa ziara hiyo ni pamoja na kampuni ya TNT ya Viet Nam kununua korosho za Tanzania kiasi cha tani 113,913.5.

116. Mheshimiwa Spika, kiongozi huyo pia alitembelea Zanzibar na kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ambapo walikubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta ya kilimo na uvuvi.

China

117. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Julai 2019 nilifanya mazungumzo na Mheshimiwa GE Huijun, Kiongozi wa Baraza la Ushauri la Bunge la Jimbo la Zhejiang la nchini China alipofanya ziara hapa nchini. Kiongozi huyo, aliambatana na wafanyabiashara kutoka kampuni 25 na viongozi 13 wa Serikali ya Zhejiang. Katika mazungumzo hayo, Tanzania na Serikali ya jimbo hilo zilikubaliana kuendelea kukuza uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na China na kuwahimiza wafanyabiashara na wawekezaji wa nchi zetu kuongeza ushirikiano wa kiuchumi kwa manufaa ya pande zote mbili.

118. *Mheshimiwa Spika*, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maazimio hayo, wafanyabiashara wa Tanzania na wale wa Jimbo la Zhejiang walifanya makongamano ya biashara Jijini Dar es Salaam na Zanzibar. Kupitia makongamano hayo, kampuni za Tanzania na Zhejiang zilisaini Hati za Makubaliano ya kuanzisha ushirikiano wa kibiashara katika maeneo ya teknolojia, mawasiliano, miundombinu, afya na madini.

119. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Lin Bin, Naibu Waziri wa Afya wa Jamhuri ya Watu wa China aliyeongoza ujumbe wa wataalam wa afya kutoka Kamisheni ya Afya ya nchi hiyo. Mheshimiwa Lin na ujumbe wake walifanya mazungumzo na uongozi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wazee na Watoto na kukubaliana kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya ushirikiano kwenye sekta ya afya kati ya Tanzania na China.

120. Mheshimiwa Spika, ujumbe huo ulipata fursa ya kutembelea baadhi ya miradi ya afya inayofadhiliwa na Serikali ya China kupitia mfuko wa fedha za misaada ikiwemo Mradi wa Kudhibiti Malaria kwa Kuuu Viluwiluwi vya Mbu wanaosababisha Malaria (*China - Tanzania Cooperation on Malaria Control*). Kufuatia Mradi huo kutekelezwa kwa mafanikio katika kata tatu za Wilaya ya Rufiji, Serikali ya China imeridhia ombi la Serikali la kuendelea kutekeleza mradi huo katika kata zilizosalia.

121. Mheshimiwa Spika, ujumbe huo pia ulitembelea Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo na Makamu wa Rais wa Hospitali ya Jimbo la

Shandong, China walisaini Makubaliano ya Ushirikiano katika Mafunzo na Matibabu ya Moyo. Makubaliano hayo yatawezesha wataalam wa afya kutoka taasisi hiyo kupata mafunzo ya matibabu ya moyo kwa kutumia vifaa vya kisasa katika hospitali ya Shandong, China. Vilevile, chini ya Mpango wa *China - Tanzania Heart to Heart Mission*, ulifanyika uzinduzi wa awamu ya pili ya kupokea madaktari wa moyo kutoka jimbo la Shandong. Katika uzinduzi huo, Hospitali ya Shandong ilitoa msaada wa vifaa tiba na dawa wenye thamani ya Dola za Marekani 200,000 kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

122. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu ziara ya wafanyabishara na wawekezaji kutoka jimbo la Shandong nchini China iliyofanyika Zanzibar. Wafanyabiashara na wawekezaji hao walifanya majadiliano na Wizara ya Biashara na Viwanda; na Wizara ya Fedha na Mipango. Katika ziara hiyo, Hati ya Makubaliano kati ya Kampuni ya Linghang Group ya China na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar ilisainiwa kwa ajili ya uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume na eneo la viwanda la Fumba.

123. *Mheshimiwa Spika*, katika kuenzi misingi iliyoasisiwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja na muasisi wa Taifa la China Hayati Mao Ze Dong, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Guo Yezhou, Naibu Waziri anayeshughulikia Masuala ya Mambo ya Nje kutoka Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) mwezi Oktoba 2019. Ziara hiyo, inaendelea kuimarisha misingi imara katika ushirikiano wa kisiasa ambao unajumuisha ziara rasmi za Viongozi Wakuu wa China na Tanzania, mawasiliano ya viongozi wa Serikali, ushirikiano wa kiuchumi na kisiasa.

124. *Mheshimiwa Spika*, katika kudumisha na kuimarisha uhusiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge la Jamhuri ya Watu wa China, mwezi Julai 2019 Wizara iliratibu ziara ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, nchini China. Katika ziara hiyo, Bunge la China liliahidi kuendeleza ushirikiano katika masuala ya kibunge.

125. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya Pili ya Kimataifa ya Bidhaa zinazotoka nje ya China (China International Importation Expo)

yaliyofanyika mwezi Novemba 2019 jijini Shanghai, China. Katika Maonesho hayo, Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi 64 zenye banda la Taifa kati ya nchi 123 zilizoshiriki. Aidha, banda la Tanzania lilikuwa miongoni mwa mabanda sita yaliyotembelewa na Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China likiwa banda pekee la nchi za Afrika lililotembelewa na kiongozi huyo ambaye alivutiwa zaidi na bidhaa ya korosho na madini ya Tanzanite. Vyombo vya habari vya nchini China vilionesha tukio hilo mubashara ambapo inakadiriwa lilitazamwa na watu wapatao milioni 100 ulimwenguni.

126. Mheshimiwa Spika, kupitia maonesho hayo, jumla ya kampuni 3,000 kutoka duniani kote zikiwemo kampuni 10 kutoka Tanzania zilishiriki kwa ajili ya kuonesha bidhaa zake kwenye soko la China. Banda la Tanzania lilitembelewa na takribani wageni 6,000 ambao walivutiwa na bidhaa za korosho, kahawa, karafuu, chai, ufuta, unga wa muhogo, mazao ya misitu, vito vilivyotengenezwa kwa madini ya Tanzanite, dhahabu, *saphire, rubby, spinel, tsavorite* na *tourmaline* na bidhaa za ngozi. Vilevile, katika banda hilo, vivutio vya utalii vya Tanzania vilioneshwa kupitia picha za mnato na *video*.

127. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu mapokezi ya kundi la watalii 120 kutoka Hong Kong, China ambao walizuru Tanzania mwezi Julai 2019 na kutembelea Mbuga za Wanyama za Serengeti na Ngorongoro. Ujumbe wa watalii hao ulijumuisha wafanyabiashara 20 ambao walipata fursa ya kufanya mazungumzo na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA) na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kwa ajili ya kupata taarifa kuhusu fursa za uwekezaji na biashara zilizopo nchini.

Indonesia

128. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu mafunzo ya usindikaji nafaka, mazao ya mizizi, matunda na mbogamboga yaliyofanyika mkoani Mbeya kwa ufadhili wa Serikali ya Indonesia. Mafunzo hayo ni sehemu ya mpango wa nchi hiyo kuleta wakufunzi kwa ajili ya kutoa elimu katika usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuyaongezea thamani na kupunguza upotevu baada ya mavuno. Kupitia mafunzo hayo, Watanzania 40 wameweza kujengewa uwezo wa usindikaji na uhifadhi wa vyakula mbalimbali.

129. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Kwanza la Viwanda kati ya Tanzania na Indonesia lililofanyika jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo lililenga kukuza wigo wa biashara ya moja kwa moja kati ya pande mbili pamoja na kufungua fursa za uwekezaji kati ya Tanzania na Indonesia. Katika kongamano hilo, wawekezaji 21 kutoka kampuni 10 za Indonesia walioshiriki walifanya mazungumzo na Taasisi za Umma na binafsi za Tanzania.

130. *Mheshimiwa Spika*, miongoni mwa mafanikio yaliyotokana na kongamano hilo ni pamoja na Kampuni ya Indesso na Kampuni ya *CV Ocean Fresh* za Indonesia kusaini Makubaliano ya Ushirikiano wa Kibiashara na Shirika la Biashara la Taifa – Zanzibar katika kuanzisha viwanda viwili vya kuzalisha mafuta yanayotokana na majani ya mimea pamoja na kuchakata zao la mwani. Tayari kiwanda cha kuzalisha mafuta kimeshaanza uzalishaji tangu mwezi Februari 2020.

131. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Tamasha la Miundombinu kati ya Indonesia na Afrika lililofanyika kisiwa cha Bali nchini Indonesia.

Wakati wa Tamasha hilo, Hati ya Makubaliano ya Ujenzi wa Bandari ya mafuta na gesi Mangapwani na Bandari ya Mpigaduri Unguja ilisainiwa kati ya Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar na Kampuni ya PT. WIKA pamoja na Benki ya EXIM ya nchini Indonesia. Makubaliano hayo yataiwezesha Zanzibar kupata mkopo wa Dola za Marekani milioni 190 kwa ajili ya ujenzi wa bandari hizo.

132. Mheshimiwa Spika, Wizara pia iliratibu ziara ya Mheshimiwa Luhut Binsar Pandjait, Waziri wa Masuala ya Bahari na Uwekezaji wa Indonesia, mwezi Desemba 2019. Lengo la ziara hiyo lilikuwa kukuza na kuimarisha juhudi za uwekezaji kati ya Tanzania na Indonesia. Kiongozi huyo alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo (Mb), Naibu Waziri wa Madini.

133. Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara hiyo, hati mbili za makubaliano kati ya Taasisi za Tanzania na Indonesia zilisainiwa. Makubaliano hayo ni kati ya SUMA JKT na Kampuni ya PT. WIKA ya Indonesia kuhusu kuanzisha kampuni ya ubia itakayoiwezesha SUMA JKT kutekeleza

miradi mikubwa ya miundombinu kupitia uwezo wa kifedha, utaalamu na uzoefu wa kampuni hiyo. Aidha, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na kampuni ya TIMAH ya Indonesia zilisaini Hati ya makubaliano yenye lengo la kuanzisha kampuni ya ubia ambayo itatafiti, kuchimba na kuchakata madini.

Jamhuri ya Korea

134. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu kusainiwa kwa Hati ya Makubaliano kwenye sekta ya kilimo kati ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar na Kampuni ya Kolon ya Jamhuri ya Korea ambayo inatekeleza mradi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji. Mradi huo unafadhiliwa kupitia mkopo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 50 kutoka Jamhuri ya Korea.

135. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Desemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye mkutano wa wadau wa kujadili ujenzi wa kijiji cha Tanzania ndani ya bustani ya Suncheon katika Jamhuri ya Korea uliofanyika jijini Dodoma. Mkutano huo uliandaa mpango kazi utakaofanikisha uanzishwaji wa kijiji cha Tanzania

katika bustani hiyo ambayo itaiwezesha nchi yetu kutangaza vivutio vya utalii pamoja na utamaduni wetu kwa wageni takribani milioni 10 watakaotembelea bustani hiyo kila mwaka. Kupewa eneo ndani ya Bustani ya Taifa la Jamhuri ya Korea ni heshima kubwa kwa Taifa letu.

8.1.3 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Mashariki ya Kati

Kuwait

136. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Julai 2019 Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Balozi Hamad Al-Mashaam, Msaidizi wa Mheshimiwa Sheikh Sabah Al-Khaled Al-Sabah, ambaye pia ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Kuwait iliyofanyika nchini. Kiongozi huyo alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Profesa Palamagamba J. A. M. Kabudi (Mb.), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu masuala mbalimbali ya ushirikiano kati ya Tanzania na Kuwait. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na umuhimu wa kuharakisha uwekaji saini mikataba ya kutokutoza kodi mara mbili katika uwekezaji na ushirikiano katika sekta ya mafuta na gesi. Viongozi hao

walikubaliana pia kuanzisha Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya nchi hizi mbili kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Umoja wa Falme za Kiarabu

137. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Septemba 2019 Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliyofanyika katika Umoja wa Falme za Kiarabu. Katika ziara hiyo, Rais Shein alifanya mazungumzo na Sheikh Saud Bin Alqasimi, Mtawala wa Ras Al-Khaimah kwa niaba ya Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu na alikubali kutoa msaada wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Fumba – Uwanja wa Ndege; ujenzi wa Hospitali Kuu ya Rufaa na ya kufundishia ya Binguni; ukarabati wa majengo ya Mji Mkongwe pamoja na ujenzi wa majengo ya Kitivo cha Historia na Mambo ya Kale katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Aidha, katika ziara hiyo viongozi hao walisaini Hati za Makubaliano kuhusu:

- (i) Msaada wa fedha wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 10 kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Biashara wa Khalifa kwa ajili

ya kusaidia wajasiriamali wadogo na wa kati Zanzibar; na

- (ii) Msaada wa fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni 10 kutoka Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Hospitali ya Wete iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba.

138. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Machi 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika makabidhiano ya Kituo cha Afya Paje Zanzibar kilichojengwa kwa msaada wa Serikali ya Umoja wa Falme ya Kiarabu (UAE). Aidha, pamoja na kituo hicho, nchi hiyo ilitoa msaada wa gari moja la kubebea wagonjwa na vifaa vya shule, vyote vikiwa na thamani ya Shilingi bilioni 1.38.

Qatar

139. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Madini kutoka Taifa la Qatar. Madhumuni ya ziara hiyo yalikuwa ni kuangalia fursa za kununua madini ya dhahabu pamoja na kuwekeza katika sekta ya madini, hususan uongezaji thamani dhahabu inayozalishwa nchini. Kampuni hiyo ilipatiwa

taarifa muhimu zinazoelezea taratibu za upatikanaji wa leseni na kuanzisha kampuni, taarifa za masoko ya dhahabu, sheria zinazosimamia biashara ya madini, sheria za kodi na sheria ya uwekezaji. Wizara inaendelea kuwasiliana na kampuni hiyo ili kufanikisha uwekezaji unaokusudiwa.

Israel

140. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Kongamano la Nane la Maji na Mazingira lililofanyika jijini Tel Aviv nchini Israel. Kongamano hilo lilifanyika sambamba na Maonesho ya Teknolojia mbalimbali za maji safi na maji taka. Ujumbe wa Tanzania ulipata fursa ya kufanya mazungumzo na viongozi wa Wizara na Mamlaka za Maji nchini Israel. Katika mazungumzo hayo, Serikali ya Israel iliahidi kutoa nafasi za mafunzo kwa ajili ya wataalam wa Tanzania kwenda Israel pamoja na kuleta wakufunzi hapa nchini.

141. Mheshimiwa Spika, kutokana na mahusiano mazuri yaliyopo kati ya nchi yetu na Israel, Wizara iliratibu upatikanaji wa nafasi 100 kwa ajili ya vijana wa Kitanzania kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa nchini Israel kwa ufadhili wa

nchi hiyo. Mafunzo hayo yalianza rasmi mwezi Septemba 2019 na yanatarajiwa kumalizika mwezi Agosti 2020. Ni matarajio yetu kuwa wanafunzi hao watatumia ujuzi, utaalam na uzoefu watakaoupata nchini humo kuanzisha shughuli mbalimbali za kilimo watakaporejea nchini. Vilevile, mwezi Oktoba na Desemba 2019, Wizara iliratibu ujio wa watalii 2,000 kutoka nchini Israel. Watalii hao walitembelea vivutio mbalimbali vya utalii Tanzania Bara na Zanzibar.

Oman

142. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Januari 2020, niliwasilisha ujumbe maalum wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Muadham Sultan Haitham Bin Tariq Bin Taimur Al Said, Mfalme mpya wa Taifa la Oman, kufuatia kifo cha Kiongozi wa Taifa hilo Muadham Sultan Qaboos Bin Said kilichotokea tarehe 10 Januari 2020. Nilipokuwa nchini Oman, nilipata fursa ya kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Yusuf Bin Alawi Bin Abdullah, Waziri wa Mambo ya Nje wa Oman ambaye alimshukuru Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla kwa kumtumia Sultan Haitham salamu za pole kwa kifo cha kiongozi wao na salamu za pongezi kwa kuteuliwa kwake.

Mheshimiwa Alawi aliahidi kuwa Serikali ya Oman chini ya utawala mpya itaendeleza uhusiano mzuri wa kihistoria na kidugu uliopo kati ya Oman na Tanzania ikiwemo utekelezaji wa ahadi za Hayati Sultan Qaboos Bin Said. Ziara hiyo ilikuwa muhimu kwa kuzingatia mahusiano ya kidugu na damu kati ya watu wa Oman na Tanzania ambapo wapo wa Oman waliotoka Tanzania Bara na Zanzibar.

8.1.4 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Ulaya na Amerika

Marekani

143. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Machi 2020, niliwasilisha ujumbe maalum wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Mheshimiwa Donald Trump, Rais wa Marekani. Pamoja na masuala mengine, ziara hiyo iliniwezesha kufanya mazungumzo na Mhe. Balozi Tibor Nagy, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani anayeshughulikia Masuala ya Afrika; Bi. Jennifer D. Nordquist, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia anayewakilisha Marekani; Balozi Mark Green, Mtendaji Mkuu wa Shirika la Msaada la Marekani (USAID) na Balozi Kelley E. Currie,

Balozi - Kazi Maalum (Ambassador-at-Large) anayeshughulikia Masuala ya Wanawake Duniani.

144. *Mheshimiwa Spika*, kwa ujumla ziara hiyo imekuwa na mafanikio kwani imeipa Serikali yetu nafasi ya kutoa ufafanuzi wa masuala ambayo ama yalikuwa hayaeleweki vizuri kwa wabia wetu wa maendeleo au yalikuwa yanapotoshwa kwa makusudi na baadhi ya watu au kundi la watu wasioitakia mema nchi yetu. Vilevile, kupitia ziara hiyo, nchi yetu imeongeza idadi ya watakaoisemea vizuri ama kuitetea pindi itakapokuwa ikisemwa vibaya.

145. *Mheshimiwa Spika*, kidiplomasia, kukutana na kufanya mazungumzo na viongozi hao kumeimarisha uhusiano na ushirikiano uliopo na pia kupeleka ujumbe na kuidhihirishia Jumuiya ya Kimataifa kuwa Tanzania na Marekani bado ni wabia wakubwa wanaoshirikiana vizuri katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

Poland

146. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Marcin Przydacz, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa

Poland. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano kwenye sekta ya maji ikiwemo uwezekano wa kutumia maji taka kuzalisha nishati katika jiji la Dodoma na Dar es Salaam. Kufuatia ziara hiyo, mwezi Desemba 2019, Tanzania na Poland zilisaini makubaliano ya kuanzisha ushirikiano katika sekta ya maji.

Cuba

147. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Marcelino Gonzalenz, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Cuba. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Cuba kwenye sekta za elimu, afya, utalii na kilimo. Kufuatia ziara hiyo, majadiliano ya ushirikiano katika sekta ya kilimo yameanza. Aidha, mwezi Januari 2020 Tanzania na Cuba zilisaini makubaliano ya kuleta madaktari bingwa wa mfumo wa fahamu, figo na moyo ili watoe huduma hizo katika Hospitali ya Benjamin William Mkapa iliyopo jijini Dodoma.

148. Mheshimiwa Spika, vilevile, katika ziara hiyo Mheshimiwa Gonzalenz alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa

Baraza la Mapinduzi na kukubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta za afya, kilimo, na uvuvi. Majadiliano kuhusu maeneo ya ushirikiano katika sekta hizo kwa ngazi ya wataalam yanaendelea.

Ukraine

149. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu ziara ya ujumbe wa wawekezaji wa kiwanda cha kusindika nyama cha *Saltivsky Meat Processing Plant INC* cha nchini Ukraine. Ujumbe huo ulitembelea machinjio ya Vingunguti na kukutana na Baraza la Usimamizi wa Mazingira kwa lengo la kupata taarifa na taratibu za kuanzisha kiwanda cha kusindika nyama. Ujumbe huo umeahidi kurejea nchini hivi karibuni kutembelea mikoa ya Shinyanga, Kagera na Dodoma ambayo imependekezwa kujengwa kiwanda hicho.

Uturuki

150. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu ziara ya wawekezaji, wafanyabiashara 38 na wakuu wa vyuo viwili kutoka mji wa Sakarya, Uturuki. Ujumbe huo uliongozwa na Bw. Ekrem Yuce, Meya wa Mji wa Sakarya. Kutokana na ziara hiyo, Chuo Kikuu cha

Sakarya (Sakarya University) na Chuo Kikuu cha Sayansi cha Sakarya (University of Applied Sciences) vya Uturuki vilisaini makubaliano ya ushirikiano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masuala ya utafiti katika sayansi; kubadilishana wanafunzi na wataalam pamoja na ufadhili wa masomo kwenye vyuo hivyo.

151. Mheshimiwa Spika, ujumbe huo pia ulitembelea Zanzibar na kufanya mazungumzo na Mstahiki Suleiman Kinana, Meya wa Jiji la Zanzibar kuhusu ushirikiano kati ya Jiji la Zanzibar na Jiji la Sakarya ambapo viongozi hao walisaini makubaliano ya awali ya ushirikiano (Letter of Intent) kati ya Majiji hayo. Aidha, ujumbe huo ulifanya mazungumzo na viongozi wa mamlaka za Serikali pamoja na wadau mbalimbali kwenye sekta binafsi ili kuangalia namna ya kushirikiana katika maeneo mengine ya kimkakati.

152. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara ilifanikisha ziara ya mwekezaji kutoka kampuni ya *Unit Textile* ya nchini Uturuki. Mwekezaji huyo ana nia ya kujenga kiwanda cha nguo na vyombo vya nyumbani mkoani Simiyu. Uwekezaji huo unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 50 na kutoa ajira zipatazo 2000. Mamlaka za mkoa zimempatia eneo lenye

ukubwa wa ekari 100 kufanikisha ujenzi wa viwanda hivyo. Mwekezaji huyo tayari amesajili kampuni hapa nchini itakayosimamia uwekezaji huo ijulikanayo kwa jina la *Tem Unique Simiyu Limited*.

Ubelgiji

153. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Machi 2020, Wizara ilifanikisha upatikanaji wa soko kubwa la maharage machanga ya kijani (green beans) nchini Ubelgiji. Soko hilo limepatikana baada ya kufanya mazungumzo na kampuni ya Charlier - Brabo Group - CBG inayonunua maharage hayo kutoka sehemu mbalimbali duniani. Kampuni hiyo iko tayari kununua kontena takribani 180 ya maharage yenye urefu wa futi 40 kila mwaka.

154. *Mheshimiwa Spika*, kupatikana kwa soko hili nchini Ubelgiji ni habari njema kwa wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo hususan kwa aina hii ya maharage ambayo tayari yana soko nchini Uholanzi. Tunatoa wito kwa Watanzania kuchangamkia upatikanaji wa soko hili jipya.

Uholanzi

155. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu kusainiwa kwa Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Uholanzi kwenye ufugaji wa kuku na samaki. Kufuatia makubaliano hayo mradi wa shamba darasa la ufugaji wa samaki na kuku uliopo Kigamboni, Dar es Salaam ulizinduliwa mwezi Februari 2020. Lengo la mradi huo ni kutoa mafunzo kwa Watanzania wenye nia ya kuwekeza kwenye biashara ya ufugaji wa samaki kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Mradi huu, unaendeshwa kwa ubia baina ya Serikali ya Tanzania, Kampuni ya Riga Safina ya Tanzania pamoja na Kampuni tano za Uholanzi.

8.1.5 Ushirikiano wa Kikanda

Jumuiya ya Afrika Mashariki

Mkutano wa 29 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

156. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa 29 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wanaohusika na masuala ya Afrika Mashariki na Mipango uliofanyika jijini Arusha. Pamoja na masuala

mengine, Nchi Wanachama zilitakiwa kukamilisha zoezi la kuhuisha sheria hususan sheria na vibali vya kazi ili ziendane na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ifikapo mwezi Septemba 2020.

Bunge la Afrika Mashariki

157. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu na kushiriki katika mikutano mitatu ya Bunge la Afrika Mashariki. Katika mikutano hiyo, Bunge lilijadili na kupitisha Muswada wa Sheria wa mwaka 2020 wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kiasi cha Dola za Marekani 4,977,475 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Vyombo na Taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, Bunge lilijadili taarifa za kamati na kupitisha mapendekezo ya hatua mbalimbali za kuchukuliwa na Baraza la Mawaziri ili kuimarisha maeneo ya ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Itifaki ya Umoja wa Forodha

158. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye

Mkutano wa 36 wa Dharura wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji wa Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Arusha. Mkutano huo ulipitisha Mkakati wa Miaka Kumi wa Kuendeleza Sekta ya Pamba na Nguo wa mwaka 2019 – 2029. Mkakati huo unalenga kuongeza uzalishaji wa mbegu za pamba kutoka tani 290,000 hadi tani 1,000,000 kwa mwaka na kuongeza uwezo wa kuchakata pamba na kuwa kitambaa kutoka urefu wa mita milioni 6.9 hadi kufikia urefu wa mita milioni 37.3.

159. Mheshimiwa Spika, vilevile, katika mkutano huo, Nchi Wanachama zilikubaliana kuwa ngozi iliyosindikwa kwa kiwango cha kati (wet blue) inayouzwa nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki itozwe ushuru wa asilimia 10 kuanzia mwaka 2019/2020. Aidha, kiwango hicho kitaendelea kuongezeka kwa asilimia 10 kila mwaka kwa kipindi cha miaka 10 ili kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vya kuzalisha ngozi na bidhaa za ngozi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Itifaki ya Soko la Pamoja

160. Mheshimiwa Spika, katika kuadhimisha miaka 20 ya uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika

Mashariki, Wizara iliratibu na kushiriki katika Maonesho ya Kitaifa ya Wajasiriamali wa Tanzania yaliyofanyika mwezi Oktoba 2019, mji mpya wa Fumba, Zanzibar. Kupitia maonesho hayo, wajasiriamali wapatao 250 kutoka Tanzania na Kenya walipata fursa ya kuuza na kutangaza bidhaa mbalimbali wanazozalisha.

161. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Desemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye maonesho ya 20 ya wajasiriamali Afrika Mashariki yaliyofanyika Kigali, Rwanda. Wajasiriamali wapatao 1,500 kutoka Nchi Wanachama wakiwemo 160 kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walishiriki katika Maonesho hayo. Wajasiriamali hao pia walipata fursa ya kubadilishana taarifa za kibiashara, ujuzi pamoja na huduma.

162. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Machi 2020, Wizara iliratibu Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Chama cha Wafanyabiashara wa Uswidi na Afrika Mashariki (SWEACC) lililofanyika Jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 200 kutoka nchi za Afrika Mashariki, Uswidi na Nordic kwa ujumla. Lengo la Kongamano hilo ni kuhamasisha uwekezaji na

biashara baina ya Uswidi na Nchi za Afrika Mashariki. Aidha, kongamano hilo lilitoa fursa kwa kampuni za Uswidi na Norway kutangaza matumizi na uwekezaji wa teknolojia ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na bidhaa zitakazopelekea ukuaji endelevu wa maisha bora ya wananchi wa Tanzania na Afrika Mashariki. Maeneo matatu ya kipaumbele kwenye Kongamano hilo yalikuwa ni maji na usafi wa mazingira, usafiri rafiki kwa mazingira na urejezaji taka kuwa nishati.

163. Mheshimiwa Spika, matokeo ya Kongamano hilo ni pamoja na kusainiwa Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) na Chama cha Wafanyabiashara wa Uswidi na Afrika Mashariki kuhusu ushirikiano katika kukuza uwekezaji na biashara. Vilevile, wakati wa Kongamano hilo Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) alikutana na kufanya mazungumzo na kampuni za SCANIA ambao wana lengo la kurejea nchini kuanzisha kiwanda cha kuunganisha magari.

164. Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye

Mkutano wa 13 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Kilimo na Usalama wa Chakula la Afrika Mashariki uliofanyika Arusha. Nchi Wanachama zilikubaliana kuanzisha Sera na Mikakati ya kuwahusisha vijana kikamilifu katika sekta ya kilimo kwa kuzingatia jinsia. Aidha, Mkutano huo uliziagiza Nchi Wanachama ambazo hazijaridhia Itifaki ya Afya ya Wanyama na Mimea kuridhia kabla ya mwezi Machi 2020.

165. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Kisekta la Mazingira na Usimamizi wa Maliasili la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Dodoma. Mkutano huo ulijadili na kupitisha rasimu ya Itifaki ya Mazingira na Usimamizi wa Maliasili, rasimu ya Sera ya Misitu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa utekelezaji wake pamoja na rasimu ya Mpango Kazi Kabambe kwa ajili ya kutekeleza mapendekezo yanayohusu kupunguza na kusimamia maafa.

Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki

166. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Fedha na

Masuala ya Uchumi uliofanyika Jijini Arusha. Mkutano huo, ulijadili utekelezaji wa Maamuzi ya Mkutano wa 34 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kufanya mapitio ya Mkataba wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB). Iliamuliwa kuwa Baraza la Uongozi wa Benki lizingatie mipango ya maendeleo ya Jumuiya wakati wa kuandaa vipaumbele vya Benki hiyo. Vilevile, iliamuliwa kuweka ukomo wa muda wa nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Benki kama ilivyo kwenye benki nyingine za kikanda. Aidha, Mkutano huo ulipitisha rasimu ya Sera ya Benki ya Afrika Mashariki na Mkakati wa Utekelezaji wake.

Masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama

167. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika zoezi la pamoja la vituo vya uamrishaji vya majeshi ya Nchi Wanachama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (CPX USHIRIKIANO IMARA) lililofanyika Jinja, Uganda. Lengo la zoezi hilo ni kuyajengea uwezo majeshi yetu katika kukabiliana na ugaidi, uharamia, maafa na urejeshaji wa amani wakati wa machafuko. Zoezi hilo lilihusisha jumla ya washiriki 360 kutoka majeshi ya ulinzi, polisi na

Asasi za kiraia kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

168. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inaendelea na uratibu wa maandalizi ya rasimu ya Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni hatua ya mpito kuelekea Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Timu ya wataalam iliyoundwa kwa ajili ya kuandaa rasimu ya Katiba ya Fungamano kama ilivyoagizwa kwenye Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi Wanachama, imeanza kukusanya maoni ya wadau katika Nchi Wanachama yatakayoweza kupendekeza modeli ya Fungamano na maeneo ya ushirikiano.

169. *Mheshimiwa Spika*, zoezi la kukusanya maoni ya wadau lilianza mwezi Januari 2020 nchini Burundi na litaendelea katika nchi nyingine za Jumuiya. Kwa upande wa Tanzania, zoezi hilo linatarajiwa kufanyika mwezi Agosti 2020. Naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kujitokeza kwa wingi wakati wa zoezi hilo.

170. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwenye Tamasha la Michezo na

Utamaduni kwa Majeshi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika Jijini Nairobi, Kenya. Tamasha hilo lilifanyika kama sehemu ya jitihada za kuimarisha ushirikiano na kujenga kuaminiana miongoni mwa askari wa majeshi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

171. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Ushirikiano katika sekta ya Ulinzi uliofanyika jijini Arusha. Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulijadili na kupitisha mapendekezo ya kuanzisha Kituo cha Kikanda cha Kuratibu Mapambano dhidi ya Ugaidi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni kuendeleza juhudi za mapambano dhidi ya ugaidi kwenye Jumuiya hiyo.

172. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha utawala bora na uwajibikaji kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara iliratibu ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusiana na Rasimu ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Maoni ya Tanzania kuhusiana na rasimu ya Itifaki hiyo yamewasilishwa Seketarieti ya Jumuiya.

Programu za Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Kijamii

173. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Oktoba 2019 Wizara iliratibu ufunguzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani Tunduma/Nakonde kilichopo katika mpaka wa Tanzania na Zambia. Kituo hicho kilizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Edgar Chagwa Lungu, Rais wa Jamhuri ya Zambia. Uwepo wa kituo hicho katika mpaka huo umerahisisha shughuli za kibiashara kati ya Tanzania na Zambia.

174. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuratibu zoezi la kutoa mafunzo kwa watumishi wa Serikali waliopo katika vituo vinane vya Huduma za Pamoja Mipakani ambavyo ni Holili / Taveta (Tanzania / Kenya); Mutukula / Mutukula (Tanzania / Uganda); Rusumo / Rusumo (Tanzania / Rwanda); Kabanga / Kobero (Tanzania / Burundi); Namanga / Namanga (Tanzania / Kenya); Sirari / Isebania (Tanzania / Kenya); Horohoro / Lungalunga (Tanzania / Kenya); na Tunduma / Nakonde (Tanzania / Zambia) ili kuwezesha kutoa huduma zinazostahili kwa watumiaji wa vituo hivyo. Aidha, Wizara

inaendelea kutoa elimu kwa umma ili kuwawezesha kufahamu huduma zinazotolewa na vituo hivyo na kutumia fursa zilizopo kikamilifu.

175. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Pili wa Mawaziri wa Sekta za Miundombinu wa COMESA, EAC na SADC uliofanyika Lusaka, Zambia. Katika Mkutano huo, pamoja na masuala mengine, nchi hizo zilikubaliana kutokuwa na ongezeko la uzito wa jumla wa magari ya kusafirisha mizigo unaoruhusiwa kwa lengo la kulinda miundombinu ya barabara; kuboresha mifumo ya kitaasisi ya utekelezaji wa Programu ya Kuwezesha Sekta ya Uchukuzi na Biashara kwa Nchi Wanachama; kuwianisha mifumo ya kudhibiti uzito wa magari na usajili wa leseni kwa vyombo vya usafiri kwa njia ya barabara; na kuwianisha mifumo ya usajili wa watoa huduma za usafirishaji na mfumo wa pamoja wa kielektroniki wa kusajili watoa huduma za usafirishaji kwa nchi zote wanachama.

176. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 18 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Nairobi, Kenya. Pamoja na masuala mengine,

mkutano huo ulijadili utekelezaji wa Programu ya kuhuisha taratibu za udhibiti wa dawa na vifaa tiba katika Nchi Wanachama. Mkutano huo ulikubaliana taratibu za usajili wa dawa na ukaguzi wa pamoja zifuate miongozo iliyokubalika ili kudhibiti dawa zisizokuwa na ubora zinazozalishwa na Nchi Wanachama pamoja na zile zinazoingizwa ndani ya Jumuiya.

177. *Mheshimiwa Spika*, Mkutano huo pia, ulijadili utekelezaji wa Mradi wa Maabara Maalumu Zinazotembea kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko na kuambukiza. Mradi huo, unahusisha kuingizwa kwa vifaa tiba vya maabara kutoka kwa wazabuni mbalimbali duniani kupitia bandari au viwanja vya ndege vya Nchi Wanachama. Tanzania ilikubali vifaa vya mradi huo vipitie katika bandari ya Dar es Salaam na katika viwanja vyake vya ndege. Baadhi ya vifaa hivyo vimeshapokelewa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na tayari zimesambazwa katika Nchi Wanachama.

178. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu Tamasha la Nne la Jumuiya ya Afrika Mashariki la Utamaduni lijulikanalo kama Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni *Festival*

(JAMAFEST) lililofanyika jijini Dar es Salaam ikiwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa Tamasha hilo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2013. Tamasha hilo limekuwa likifanyika kwa mzunguko kila baada ya miaka miwili katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tamasha hilo lilifunguliwa rasmi na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufungwa rasmi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Lengo la Tamasha hilo ni kukuza utamaduni wa jamii za watu wa Afrika Mashariki ambapo maonesho mbalimbali ya kiutamaduni ikiwemo mavazi ya asili, sanaa ya uchongaji, michezo ya kuigiza, mapishi ya vyakula vya asili na michezo ya jadi huoneshwa. Kupitia Tamasha hilo, Tanzania ilipata fursa ya kuonesha tamaduni zake pamoja na kutangaza vivutio vya utalii na utamaduni vilivyopo nchini.

179. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu ziara ya tatu ya waendesha baiskeli iliyojumuisha vijana 22 kutoka katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ziara ya namna hii imekuwa ikifanyika kila mwaka kuanzia mwaka 2016 kwa lengo la kuhamasisha michezo; kutangaza utamaduni na vivutio vya

utalii vya Nchi Wanachama; pamoja na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Ziara hiyo ilianza nchini Uganda tarehe 1 Agosti 2019 na kupita katika nchi za Kenya, Tanzania, Burundi, Rwanda na kuhitimishwa nchini Uganda tarehe 20 Septemba 2019. Aidha, waendesha baiskeli hao walipokuwa nchini, walipata fursa ya kutembelea Ofisi za balozi za Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Arusha.

180. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu mafunzo ya wawezeshaji wanawake kiuchumi kupitia mradi wa *50 Million African Women Speak Networking Platform*. Mafunzo hayo yaliyoshirikisha wanawake 40 kutoka Taasisi za Serikali na vikundi vya Asasi Zisizo za Kiserikali vinavyoratibu masuala ya maendeleo ya wanawake yalifanyika jijini Dodoma mwezi Novemba 2019. Lengo la mradi huu ni kujenga mfumo wa kidigitali wa mawasiliano baina ya wanawake ili kupata taarifa za kifedha na kupata masoko ya bidhaa zinazozalishwa na wanawake. Mradi huu unatekelezwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na kwa upande wa Zanzibar unatekelezwa chini ya

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wazee, Wanawake na Watoto.

181. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Kongamano la Kwanza la Programu ya wanafunzi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (German Development Bank - KfW) lililofanyika Entebbe, Uganda. Programu hii inafadhili wanafunzi wapatao 60 wa Nchi Wanachama wenye mahitaji maalum (poor and disadvantaged) wanaosoma masomo ya Hisabati; Uhandisi; Sayansi na Teknolojia; na masomo ya Sayansi ya Biashara kwa ngazi ya shahada ya uzamili na stahada ya uzamili kwenye vyuo vilivyopo ndani ya Jumuiya. Kila nchi mwanachama inatoa idadi sawa ya wanafunzi 10 watakaogharamiwa mafunzo hayo. Kwa upande wa Tanzania, vyuo vinavyopokea ufadhili huo ni Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na Chuo cha Ushirika Moshi. Idadi ya Watanzania wanaofadhiliwa kwa sasa ni 10 ambapo wanaume ni sita na wanawake wanne.

182. Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2020 Wizara iliratibu Mkutano wa Dharura wa Pamoja wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Masuala ya

Jumuiya ya Afrika Mashariki na Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya uliofanyika kwa njia ya mtandao (*Video Conference*). Mkutano huo ulitoa Azimio la mikakati ya pamoja ya kukabiliana na mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19) na mipango ya kutatua changamoto zinazojitokeza kutokana na hatua zinazochukuliwa na Nchi Wanachama katika kukabiliana na ugonjwa huo.

183. *Mheshimiwa Spika*, baadhi ya maazimio ya Mkutano huo ni: -

- i. Kutekeleza agizo la kukaa karantini kwa lazima kwa siku 14 kwa wasafiri wote wanaoingia katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- ii. Kuendesha mikutano kwa njia ya mtandao hadi hapo hali ya maambukizi itakapodhibitiwa;
- iii. Kuhakikisha malori yanayobeba bidhaa yanakuwa na wafanyakazi wawili hadi watatu tu; na

iv. Kuwapima wafanyakazi (*Crew*) wa malori na endapo mmoja wao atapatikana na dalili za ugonjwa wa COVID-19 wataatengwa (quarantined) kwa muda wa siku 14 kulingana na miongozo ya kitaifa na nchi husika na lori hilo litapuliziwa dawa kabla ya kuendelea na safari na wafanyakazi wengine.

184. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza Azimio la Mkutano wa Pamoja wa Dharura wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya, Tanzania ni kiungo muhimu cha usafirishaji wa bidhaa kwa baadhi ya Nchi Wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC. Katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona, imeendelea kuacha mipaka yake wazi kwa kuruhusu bidhaa muhimu kuelekea katika nchi zisizo na bandari kupita. Corona ni hatari, lakini kukosekana kwa mahitaji muhimu kwa nchi zisizo na bandari kama chakula, dawa na mafuta ya petroli ambavyo vinapitia katika bandari yetu kuelekea katika nchi zisizo na bandari kunaweza kuwa ni hatari zaidi.

185. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza hilo, tumezielekeza mamlaka zetu za vituo vya pamoja mipakani (OSBPs) kuhakikisha

wanaepusha vikwazo visivyo vya lazima kwa kukaa pamoja na wenzao wa nchi jirani waliopo katika vituo hivyo kutatua changamoto za mipakani katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Corona bila kuathiri upatikanaji wa bidhaa hizo muhimu katika nchi zisizo na bandari.

186. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki iliratibu ujenzi wa barabara za: Arusha - Namanga- Arthi River (km 240) ambapo Tanzania ina kipande cha kilomita 104.4 uliogharimu Dola za Marekani milioni 63.2; Arusha – Holili/Taveta-Voi (km 260). Ujenzi wa awamu ya kwanza kwa upande wa Tanzania unaohusisha upanuzi wa barabara ya Sakina – Tengeru (km 42) kuwa njia nne na ujenzi wa barabara ya mzunguko (Arusha Bypass) ulikamilika kwa gharama ya Shilingi 183,710,845,663.

187. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara inaendelea kuratibu ukamilishwaji na upatikanaji wa fedha za miradi ya barabara za: Lusahunga – Rusumo/Kayonza kwa kipande cha Tanzania. Upembuzi yakinifu wa kipande hicho umekamilika na gharama za mradi zitajulikana baada ya usanifu wa kina; Nyakanazi - Kasulu –Kidahwe - Mpanda unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani

milioni 373; Malindi – Mombasa – Lungalunga/Horohoro – Tanga – Pangani – Bagamoyo (km 178) kwa upande wa Tanzania ujenzi wa kipande cha Tanga - Pangani - Bagamoyo utagharimu kiasi cha Dola za Marekani milioni 195.5; na Kumunazi – Kasulu/Bukene na ukarabati wa Kyaka – Mutukula (km 252.5) upembuzi yakinifu umekamilika na usanifu wa kina umeanza ili kupata gharama za mradi.

Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

188. *Mheshimiwa Spika*, kama nilivyoeleza kwenye sehemu ya mafanikio ya Wizara kwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano kuwa Tanzania ni mwenyekiti na mwenyeji wa mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Agosti 2019 hadi Agosti 2020. Katika kipindi cha uenyekiti wetu tumejiwekea vipaumbele mbalimbali ikiwemo: uendelezaji wa viwanda; matumizi bora ya rasilimali fedha za Jumuiya; kuondolewa kwa vikwazo vya kiuchumi kwa nchi ya Zimbabwe; na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Jumuiya.

189. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Wizara imeratibu kwa mafanikio makubwa na kufanikisha kufanyika kwa Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika tarehe 18 Machi 2020. Mkutano huo ulifanyika kwa mara ya kwanza kwa njia ya mtandao ikiwa ni tahadhari dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID 19).

190. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na masuala mengine Mkutano uliazimia yafuatayo: -

- i) Kuendesha mikutano kwa njia ya mtandao hadi hapo hali ya maambukizi itakapodhibitiwa;
- ii) Kupitisha pendekezo la kuzindua shughuli za maadhimisho ya miaka 40 ya SADC;
- iii) Kuunga mkono pendekezo la Umoja wa Afrika la kuwa na mgombea mmoja kutoka Afrika katika nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani; na
- iv) Kuridhia Dira ya SADC ya mwaka 2050 na Mpango Mkakati Elekezi wa Maendeleo ya Kikanda na kuelekeza iwasilishwe kwenye

Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kwa maamuzi.

191. Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kutekeleza majukumu yake ya uenyekiti wa SADC ambapo katika kipindi hiki tumeendelea kutekeleza ajenda ya mtangamano wetu na kuhakikisha kuwa malengo ya Jumuiya yanafikiwa kama yalivyoainishwa katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, ambapo tumekuwa tukiongozwa na nyaraka mbili za kimkakati ambazo ni Mpango Mkakati Elekezi wa Kanda (RISDP) wa mwaka 2015 – 2020 na Awamu ya Pili ya Mpango Mkakati wa Asasi za Siasa, Ulinzi na Usalama (SIPO II). Mipango mikakati hii inafikia ukomo wake mwaka 2020. Hivyo, kama ilivyoelekezwa na Wakuu wa Nchi na Serikali na Jumuiya hiyo, Sekretarieti imeanza uratibu wa maandalizi ya mipango mikakati mingine itakayopelekea kutekeleza ajenda ya mtangamano wa Jumuiya baada ya mwaka 2020.

192. Mheshimiwa Spika, ni furaha kubwa kwamba mikakati hii inaandaliwa wakati wa uenyekiti wetu ambapo kukamilika kwake itakuwa ni kukamilika kwa moja ya jukumu katika uenyekiti wetu. Aidha, tumeendelea kusimamia masuala

muhimu ya maendeleo ya Jumuiya kwa kuzingatia Kaulimbiu yetu ya “Mazingira Wezeshi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu na Jumuishi ya viwanda; kukuza biashara na ajira ndani ya SADC”. Hata hivyo, pamoja na jitihada zote za kuhakikisha kuwa tunafikia malengo tuliyojiwekea, kipindi hiki kimekuwa kigumu kutokana na athari kubwa inayosababishwa na ugonjwa huu wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19).

193. Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 duniani, ni dhahiri kwamba ili kukabiliana nao kunahitajika ufanisi na ushirikiano wa hali ya juu katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa. Kufuatia hali hiyo, kwa mara nyingine tena naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa SADC pamoja na Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Katibu Mtendaji wa SADC kwa maelekezo na ushauri wanaoendelea kuutoa kwa Nchi Wanachama ili kuhakikisha kwamba ukanda wetu hauathiriki sana na janga hili la COVID-19.

194. Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mara tu

baada ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kutangaza kuwa ugonjwa huu ni janga la dunia hatukuzembea na mara moja chini ya uenyekiti wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatua mbalimbali zilianza kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa tishio kubwa linaloletwa na ugonjwa wa COVID-19 halizoroteshi shughuli za kiuchumi katika ukanda wa Jumuiya yetu endapo kasi ya maambukizi ya virusi hivyo itaongezeka. Tunafahamu fika kuwa ni jukumu letu kuhakikisha kuwa mwenendo wa uchumi, biashara, uwekezaji, na masoko ya fedha hauyumbi kutokana na athari za ugonjwa huu. Kwa hali hiyo, Nchi Wanachama zinaendelea kutathmini madhara ya kiuchumi yanayosababishwa na ugonjwa huu na kutunga sera zitakazosaidia sekta zinazohitaji zaidi msaada wa kiutawala au kifedha.

195. Mheshimiwa Spika, katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu zifuatazo ni hatua mbalimbali ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikisha. Hatua hizo ni kufanyika kwa Mkutano wa Dharura wa Mawaziri wa Afya wa SADC kuhusu COVID -19 tarehe 9 Machi 2020 chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mkutano huu ulifanyika kwa njia ya mtandao ikiwa ni hatua mojawapo ya

kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo. Mkutano huo pamoja na mambo mengine, ulipendekeza kuundwa kwa Kamati ya Wataalam kwa ajili ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Itifaki ya Afya ya SADC kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19). Mapendekezo hayo ya Mawaziri wa Afya, yaliridhiwa na Baraza la Mawaziri wa SADC katika mkutano uliofanyika tarehe 18 Machi, 2020. Aidha, tarehe 31 Machi 2020, Kamati ya Wataalam ilifanya kikao kwa njia ya mtandao na kwa kushirikiana na Sekretarieti ya SADC ilipendekeza kuandaliwa kwa mkutano huu wa Dharura wa Baraza la Mawaziri. Aidha, Kamati hiyo pia iliridhia mapendekezo 11 katika maeneo yafuatayo:

- i. Ufuatiliaji na utekelezaji wa Itifaki ya Afya kuhusu magonjwa ya mlipuko,
- ii. Kujiandaa na kukabiliana na virusi vya COVID-19;
- iii. Kubaini wagonjwa, kufuatilia waliokutana na mgonjwa na huduma za tiba;
- iv. Uzuiaji na udhibiti wa maambukizi;
- v. Uchunguzi na upimaji wa kimaabara;
- vi. Uelimishaji wa madhara na ushirikishwaji wa jamii;
- vii. Hatua stahiki za Afya ya Jamii;

- viii. Uratibu wa Kikanda wa kukabiliana na virusi vya COVID-19;
- ix. Uwezeshaji na usafirishaji wa bidhaa muhimu miongoni mwa nchi za SADC wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya COVID-19;
- x. COVID-19 na masuala ya udhibiti wa biashara katika ukanda;
- xi. Usimamizi wa majanga hatarishi katika ukanda wa SADC.

196. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 6 Aprili, 2020 niliongoza Mkutano wa Dharura wa Baraza la Mawaziri uliofanyika kwa njia ya mtandao (video conference). Mkutano huu ulijumuisha jumla ya Nchi Wanachama zifuatazo; Angola, Botswana, Eswatini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Msumbiji, Mauritius, Namibia, Seychelles, Zambia na Tanzania. Mkutano huo ulipokea taarifa ya Kamati ya Wataalam ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Itifaki ya Afya ya SADC kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 pamoja na mwongozo wa Urazinishaji (harmonisation) na uwezeshaji wa usafirishaji wa bidhaa muhimu na huduma katika nchi za SADC katika kipindi hiki cha janga la COVID -19.

197. *Mheshimiwa Spika*, Mwongozo huu unawezesha usafirishaji wa bidhaa muhimu na huduma katika nchi za SADC hatua ambayo inasaidia kuzuia kuenea kwa COVID -19 kupitia usafirishaji mipakani, kuwezesha utekelezaji na mikakati ya kitaifa ya kudhibiti kuenea kwa COVID-19, kuwezesha upatikanaji wa bidhaa muhimu kama vile mafuta, chakula na dawa, kuzuia usafirishaji usio wa lazima wa abiria kupitia mipakani na vile vile kurazinisha na kuratibu sera, kanuni na hatua za haraka za kitaifa za kukabiliana na COVID-19.

198. *Mheshimiwa Spika*, hatua hii imetokana na kasi ya maambukizi na vifo vinavyoendelea kutokea na tayari vimeanza kuleta athari hasi katika kanda yetu. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Afya Duniani ya tarehe 6 Mei 2020, idadi ya visa ni 9,841 na idadi ya vifo ni 224 katika Ukanda wa SADC kwa nchi 15 isipokuwa Falme ya Lesotho ambayo hadi sasa haina kisa hata kimoja cha maambukizi.

199. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua nyingine Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa SADC ameendelea kuzisisitizia na kuwaomba Washirika wa Maendeleo pamoja na

Taasisi za Fedha za Kimataifa kuzifutia madeni na kutoa fedha za dharura kwa Nchi Wanachama wa SADC ili kuzisaidia katika kukabiliana na athari hasi za kiuchumi zinazosababishwa na ugonjwa wa COVID-19. Wito huu wa Mheshimiwa Rais kwa niaba ya Nchi Wanachama wa SADC unaongezea uzito wito alioutoa tarehe 22 Aprili 2020, wakati alipozungumza na Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kuhusu juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya COVID – 19 na kuzitaka Jumuiya, Taasisi na Washirika wa Maendeleo watoe msamaha wa madeni kwa nchi zetu ili ziweze kutumia fedha ambazo zingelipia madeni hayo kukabiliana na janga hili la COVID-19.

200. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa nchi za SADC wanaohusika na Menejimenti ya Athari za Maafa uliofanyika Zanzibar. Mkutano huo ulifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Katika Mkutano huo, Mawaziri waliidhinisha mapendekezo ya Mapitio ya Mkakati wa Kikanda wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa Mwaka 2016 – 2030, ili uwiane na Ajenda ya mwaka 2030 ya Malengo ya Maendeleo

Endelevu, Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063 na Programu ya Utekelezaji wa Mkakati wa Sendai katika Afrika.

201. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, niliongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa 21 wa Mawaziri wenye dhamana ya Mambo ya Nje, Mambo ya Ndani na Ulinzi pamoja na Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika jijini Lusaka Zambia. Katika Mkutano huo, Nchi Wanachama ziliazimia kuendelea kuimarisha ushirikiano kwenye nyanja za siasa, demokrasia, ulinzi na usalama; na kuifahamisha Serikali ya Burundi kuhusu tathmini iliyofanyika ya maombi ya nchi hiyo kujiunga na SADC.

202. Mheshimiwa Spika, vilevile, mkutano huo uliiteua Jamhuri ya Zimbabwe kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya SADC ya Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama; kuziteua nchi za Tanzania, Angola, Botswana, DRC, Malawi na Afrika Kusini kwa kushirikiana na Sekretariati ya SADC na Ofisi ya Kikanda ya *Interpol* iliyopo Harare, Zimbabwe kuandaa rasimu ya Mkakati na Mpango Kazi wa

SADC unaohusika na silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi.

203. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa pamoja wa Mawaziri wa Afya na Mawaziri wenye dhamana ya VVU na UKIMWI wa SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulijadili hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Itifaki ya Afya ya SADC ya mwaka 1999 na Mpango Mkakati wake na kuridhia maazimio mbalimbali kuhusu masuala ya afya.

204. Mheshimiwa Spika, wajumbe wa mkutano huo walipata fursa ya kutembelea maeneo ya kimkakati ikiwemo kiwanda cha viuadudu vya malaria cha *Labiofarm* kilichopo Kibaha mkoani Pwani. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kutangaza bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho. Kadhalika, Mawaziri hao walitembelea Bohari ya Dawa (*msd*) ikiwa ni mkakati wa kutangaza shughuli zake kwa Nchi Wanachama kufuatia ushindi wa zabuni ya ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa na vifaa tiba kupitia Mpango wa SADC wa ununuzi wa pamoja.

205. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano

wa Dharura wa Mawaziri wanaounda TROIKA Mbili za SADC pamoja na nchi zinazochangia vikosi vya kulinda amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo uliofanyika jijini Dar es Salaam. Katika Mkutano huo, DRC ilishiriki kama mjumbe mwangalizi. Mkutano huo uliazimia kuwa iwapo Misheni ya Umoja wa Mataifa ya Ulinzi wa Amani nchini DRC (MONUSCO) haitaongezewa muda ifikapo mwaka 2022, kikosi cha dharura cha SADC kiwe tayari kuchukua na kuendeleza jukumu la MONUSCO.

206. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Pamoja wa Mawaziri wanaosimamia Sekta za Mazingira, Maliasili na Utalii wa SADC uliofanyika jijini Arusha. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo uliazimia kuwa Nchi Wanachama zisaini na kuridhia Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu mapema iwezekanavyo na kuchukua hatua stahiki kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya misitu. Aidha, Mkutano huo, uliazimia Nchi Wanachama kushirikiana katika mapambano dhidi ya ujangili kwa kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Ujangili wa Nchi za SADC.

207. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Pamoja wa Mawaziri wa TEHAMA, Habari, Uchukuzi na Hali ya Hewa wa SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo uliazimia kuimarisha upatikanaji wa huduma za mtandao wenye kasi; kuanzisha mradi wa satelaiti ya pamoja; matumizi ya teknolojia ya malipo kwa njia ya kielektroniki; kupunguza gharama za huduma ya kuunganisha mawasiliano ya simu za mkononi miongoni mwa Nchi Wanachama; kuanzisha Kituo cha Kukabiliana na Uhalifu wa Kimtandao; na kuwianisha sheria, kanuni na viwango vinavyohusu masuala ya usimamizi na udhibiti wa uzito wa magari katika ukanda wa SADC.

Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu

208. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza Itifaki ya Kupambana na Unyanyasaji wa Kijinsia Dhidi ya Wanawake na Watoto ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (International Conference on the Great Lakes Region - ICGLR), mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu mafunzo ya kuzijengea uwezo Taasisi za Afya, Sheria na Jeshi la Polisi za Tanzania yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. Mafunzo hayo, yalilenga kuziongezea

Taasisi hizo ujuzi wa kukabiliana na ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa kuandaa wakufunzi watakaokuwa chachu ya kutoa elimu kwenye Taasisi zao na jamii kwa ujumla.

209. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika Brazzaville, Jamhuri ya Kongo. Katika Mkutano huo, pamoja na masuala mengine, Mkutano uliridhia pendekezo la Tanzania la kutaka Kiswahili kuanza kutumika katika mikutano na shughuli nyingine za Jumuiya hiyo na kuagiza suala hilo liwasilishwe katika kikao kijacho cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa ICGLR kwa maamuzi.

210. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa uwekezaji katika sekta ya madini wa nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika jijini Dar es Salaam. Katika mkutano huo, Tanzania ilizindua rasmi Hati ya Uhalisia wa Madini kwa lengo la kudhibiti uvunaji na usafirishaji holela wa madini nje ya nchi kulingana na miongozo na taratibu za ICGLR. Aidha, Tanzania ilitumia mkutano huo kutangaza fursa zilizopo katika sekta ya madini.

Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Bahari ya Hindi (IORA)

211. Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 19 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Bahari ya Hindi (IORA) uliofanyika Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu. Mkutano huo, uliridhia maombi ya Tanzania ya kujiunga katika makundi manne kati ya tisa yaliyopo kwenye mpango kazi wa IORA ambayo ni ulinzi na usalama wa bahari; biashara na uwekezaji; usimamizi wa uvuvi; pamoja na utalii na kubadilishana utamaduni. Aidha, Mkutano ulikubali Taasisi ya *Western Indian Ocean Marine Science Association* (WIOMSA) ya Tanzania kupewa hadhi ya uangalizi katika IORA.

Umoja wa Afrika (AU)

212. Mheshimiwa Spika, Wizara iliandaa na kushiriki katika mikutano na shughuli mbalimbali za Umoja wa Afrika kwa lengo la kuunga mkono dhana ya umajumui na harakati za ukombozi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii wa Bara la Afrika kama ifuatavyo:

213. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 12 wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) uliofanyika jijini Niamey, Niger. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano huo. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo ulizindua mifumo itakayosaidia utekelezaji wa Mkataba huo.

214. *Mheshimiwa Spika*, mifumo hiyo ni: mfumo wa kutoa taarifa, ufuatiliaji na uondoshaji wa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiushuru; mfumo wa kuhifadhi takwimu za biashara wa Afrika; mfumo wa kimtandao wa kubadilishana taarifa, kujadili mapendekezo juu ya ufunguzi wa biashara ya bidhaa; na mfumo wa kimtandao katika tovuti na programu kwa ajili ya taarifa za kibiashara katika Eneo Huru la Biashara la Afrika.

215. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika, mwezi Oktoba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kwanza wa Mawaziri

kutoka Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika wanaosimamia biashara uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia. Mkutano huo ulipitisha kanuni zitakazoongoza Baraza la Mawaziri la AfCFTA na kuielekeza Kamisheni ya Umoja wa Afrika kushirikiana na Serikali ya Ghana katika kuanzisha Sekretarieti ya kudumu ya AfCFTA.

216. Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 33 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano huo. Mkutano ulipokea taarifa ya mwaka ya Hali ya Amani na Usalama na Utekelezaji wa Mkakati wa Kusitisha Matumizi ya Silaha Barani Afrika pamoja na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na migogoro katika nchi za Sudan, Sudan Kusini, Libya, Eneo la Sahel na Pembe ya Afrika.

217. Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huo, suala la ugaidi lilitajwa kuwa tishio Barani Afrika hususan eneo la ukanda wa Sahel; Pembe ya Afrika; na Bonde la Mto Chad. Aidha, ilielezwa

kuwa mabadiliko ya tabianchi ni tishio lingine la usalama kutokana na mvua kubwa, ukame na vimbunga vinavyosababisha vifo, uharibifu wa miundombinu, mali na njaa. Aidha, Mkutano ulisisitiza umuhimu wa kuwa na jeshi la Afrika litakalopambana na ugaidi pamoja na umuhimu wa nchi za Afrika kushirikiana katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, mkutano ulilaani mataifa ya kigeni yanayoingilia mambo ya ndani ya Afrika na ukiukwaji wa zuio la kuingiza silaha na kutahadharisha kuwa adhabu itatolewa kwa wale wote wanaokiuka zuio hilo.

218. *Mheshimiwa Spika*, Mkutano huo pia ulipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063 kwa Nchi Wanachama. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika taarifa hiyo, Tanzania ilitajwa kuwa miongoni mwa Nchi Wanachama zilizofanya vizuri, hususan katika maeneo ya utoaji wa huduma za nishati ya umeme, maji safi na salama, utekelezaji wa sera ya viwanda katika kuinua uchumi wa Taifa na ushiriki katika ulinzi wa amani duniani.

219. *Mheshimiwa Spika*, katika Mkutano huo Mheshimiwa Cyril Matamela Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini alichaguliwa kuwa

Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika kwa kipindi cha kuanzia Februari 2020 hadi Februari 2021. Vilevile, Bw. Wamkele Mene kutoka Afrika Kusini alipitishwa kuwa Katibu Mkuu wa kwanza wa Sekretarieti ya Eneo Huru la Biashara la Afrika.

220. Mheshimiwa Spika, Mkutano huo ulipitisha Azimio la kuzitaka Marekani na baadhi ya Nchi Wanachama za Jumuiya ya Ulaya kuiondolea nchi ya Zimbabwe vikwazo vya kiuchumi vya muda mrefu.

8.1.6 Ushirikiano wa Ubia Kati ya Tanzania na Nchi Nyingine

221. Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Saba wa Kimataifa wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD VII) uliofanyika jijini Yokohama, Japan. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati wa Mkutano huo, Serikali ya Japan ilitangaza kutenga Dola za Marekani bilioni 20 kwa ajili ya utekelezaji wa maeneo ya ushirikiano

na nchi za Afrika kwa kipindi cha miaka mitatu (2019-2021). Tanzania iliwasilisha miradi 11 kwa Serikali ya Japan kwa ajili ya kuiombea fedha za utekelezaji. Miradi hiyo imejikita katika sekta za nishati, kilimo, ujenzi wa maeneo maalum ya viwanda na mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalam wetu katika sekta hizo.

222. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika na Urusi uliofanyika mwezi Oktoba 2019 jijini Sochi, Urusi. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano huo, uliotanguliwa na kongamano la uchumi na biashara uliazimia kufufua na kuimarisha ushirikiano katika sekta za elimu, afya, ulinzi na usalama, nishati na matumizi salama ya nyuklia, miundombinu ya kisasa na kujenga uwezo kupitia uhawilishaji wa teknolojia ya kisasa.

223. Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu alieleza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo hapa nchini, vivutio vya utalii pamoja na jitihada za Serikali

katika kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara na uwekezaji. Hotuba hiyo ilionekana kumvutia sana Mheshimiwa Vladimir Putin, Rais wa Shirikisho la Urusi. Aidha, wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikutana na kufanya mazungumzo na Kampuni nane za nchini humo zinazojishughulisha na utengenezaji wa vifaa vya treni, kilimo na mitambo ya kufua umeme; utafutaji na uchakataji wa gesi na mafuta; na ujenzi wa barabara.

224. Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo yake, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizihakikishia Kampuni hizo uwepo wa mazingira mazuri ya uwekezaji, masoko na utayari wa Serikali kutoa ushirikiano kuja kuwekeza hapa nchini. Kampuni hizo zimeonesha nia ya kuja kuwekeza na kuanzisha ubia na Kampuni za hapa nchini na Kampuni tatu kati ya hizo tayari zimeanza majadiliano na Wizara za kisekta ili kukamilisha taratibu za uwekezaji huo.

225. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye sehemu ya mafanikio ya Wizara, mwezi Novemba 2019, kwa mara ya kwanza nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi za Afrika na Nordic uliofanyika jijini Dar es Salaam. Mkutano huo

uliofanyika kwa mafanikio makubwa ulifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

226. Mheshimiwa Spika, Mkutano huo, ulijadili masuala ya ushirikiano na kuainisha vipaumbele na mikakati ya ushirikiano kwenye sekta ya biashara na uwekezaji. Aidha, Tanzania ilipata fursa ya kueleza jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano katika kupambana na rushwa; udhibiti wa uchafuzi wa mazingira; pamoja na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji. Vilevile, Tanzania ilitumia uenyeji wa Mkutano huo kutangaza fursa za biashara, uwekezaji na utalii zilizopo nchini.

227. Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2019, nilimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Kundi la Afrika, Karibeani na Pasifiki (ACP) ambayo sasa inafahamika kama OACPS uliofanyika jijini Nairobi, Kenya. Katika Mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kuzishawishi Nchi Wanachama kukubaliana na masuala yafuatayo:

- i) Kujumuisha zao la korosho kwenye orodha ya mazao ya kimkakati ndani ya ACP ambayo yatanufaika na Programu ya Mnyororo wa Thamani wa ACP. Programu hii, iliyotengewa kiasi cha Euro milioni 140 itatoa fursa kwa wakulima kupata mikopo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji, kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
- ii) Kufanya maboresho muhimu katika Mkataba wa Georgetown ulioanzisha Kundi hilo kwa kuondoa vifungu visivyokuwa na maslahi kwa Tanzania na ACP kwa ujumla;
- iii) Kujumuisha suala la kuondolewa vikwazo vya kiuchumi kwa nchi ya Zimbabwe kwenye Azimio la Nairobi na hivyo kuongeza msukumo na mshikamano wa kimataifa katika kusukuma mbele wito wa SADC;
- iv) Kuandaa vigezo mahsusi, mwongozo na kanuni za kuongoza majadiliano ya kisiasa kati ya nchi za ACP na Umoja wa Ulaya; na
- v) ACP kufanya maridhiano na Umoja wa Ulaya kwa kuzingatia hoja za msingi za nchi za ACP katika maeneo tata ambayo ni

kikwazo kwa baadhi ya nchi ikiwemo Tanzania.

228. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Januari 2020, Wizara iliratibu Maadhimisho ya Miaka 40 ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU) yaliyofanyika Makao Makuu ya Umoja huo jijini Arusha. Maadhimisho hayo, yalikusisha uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya PAPU litakalomilikiwa kwa pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Uwepo wa Makao Makuu ya PAPU hapa nchini unatoa fursa za ajira kwa Watanzania; na kuwa mwenyeji wa mikutano ya umoja huo nchini pamoja na mafunzo kwa wataalam wa Tanzania ili kuimarisha utoaji wa huduma za posta.

8.1.7 Ushirikiano wa Kimataifa

229. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Septemba 2019, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 63 wa Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) uliofanyika jijini Vienna, Austria. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo ulijadili usalama wa matumizi ya mionzi ya nyuklia na ushirikiano wa kiteknolojia katika sekta mbalimbali ikiwemo afya na kilimo. Ili kuhakikisha Tanzania inanufaika na teknolojia ya nyuklia katika sekta

hizo, ujumbe wa Tanzania ulifanya vikao na uongozi pamoja na wataalam wa shirika hilo pembezoni mwa Mkutano huo. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika vikao hivyo ni pamoja na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini inayotumia sayansi na teknolojia ya nyuklia katika sekta za afya, kilimo, maji na mifugo.

230. Mheshimiwa Spika, ujumbe wa Tanzania uliufahamisha Uongozi wa IAEA mpango wa Serikali wa kuongeza vifaa vya uchunguzi na tiba katika Hospitali ya Mnazi Mmoja – Zanzibar, Hospitali ya KCMC- Kilimanjaro na Hospitali ya Rufaa Mbeya, ili kuongeza wigo wa utoaji huduma ya uchunguzi na tiba ya maradhi ya saratani nchini. Aidha, ujumbe ulielezea azma ya Serikali ya kujenga jengo la maabara ya utafiti wa nyuklia na *Multipurpose Radiator* katika Chuo Kikuu cha Nelson Mandela kwa lengo la kupatiwa msaada wa vifaa na kujengewa uwezo wataalam wetu. Utekelezaji wa miradi hiyo unalenga kuzalisha *radioisotopes, radiopharmaceuticals* na kuhifadhi nafaka na vyakula vinavyozalishwa nchini kwa njia ya *irradiation*. Uongozi wa IAEA uliahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania kwa kutoa vifaa na kuwajengea uwezo wataalam wetu.

231. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano Mkuu wa 40 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni uliofanyika Paris, Ufaransa mwezi Novemba 2019. Katika Mkutano huo, Tanzania iliungana na nchi nyingine kuisisitiza matumizi sahihi ya teknolojia na kuimarisha ushirikiano baina ya Nchi Wanachama kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Sanjari na Mkutano huo, kulifanyika Jukwaa la Mawaziri wa Utamaduni ambapo Tanzania ilieleza jitihada za Serikali katika kutunza urithi unaoshikika na usioshikika; kuimarisha biashara kwenye bidhaa za kiutamaduni; kukuza viwanda vinavyotokana na ubunifu wa kiutamaduni; na kuheshimu uwepo wa tamaduni mbalimbali katika jamii.

232. *Mheshimiwa Spika*, juhudi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili hazikuishia tu kwenye Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SADC Region). Wizara yangu kupitia Ubalozi na Uwakilishi wetu wa Kudumu katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) mjini Paris, Ufaransa, umeanza mazungumzo na Shirika hilo ili lugha ya Kiswahili iweze kutambuliwa rasmi na kuwa miongoni mwa lugha za kimataifa zinazotumiwa na Shirika hilo.

Juhudi hizo zimeanza kuzaa matunda na tarehe 21 Februari 2020, wakati wa kusheherekea Siku ya Kimataifa ya Lugha Mama (International Mother Language Day), UNESCO kwa kushirikiana na Ubalizi na Uwakilishi wetu wa kudumu Paris, Ufaransa kwa mara ya kwanza katika historia ya kuanzishwa kwa shirika hilo, iliweza kuandaa warsha kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili na kuwaalika wataalam wa lugha kutoka Vyuu Vikuu mbalimbali kikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Hii ni mmoja ya hatua za mwanzo na nzuri katika kukipeleka Kiswahili katika Shirika hilo, na Wizara yangu inaahidi kuendelea na juhudi hizo.

233. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Tatu wa Dharura wa Umoja wa Posta Duniani uliofanyika Geneva, Uswisi mwezi Septemba 2019. Lengo la Mkutano huo lilikuwa kujadili mapendekezo ya mfumo wa malipo ya ada kwa huduma za posta kufuatia malalamiko ya Marekani kuwa mfumo unaotumika unaisababishia hasara. Katika mkutano huo, Nchi Wanachama zilikubaliana kurekebisha viwango vya ada ya kusafirisha barua, vifurushi na vipeto vinavyozingatia maslahi ya nchi zote.

234. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya ujumbe wa Timu Maalumu ya Umoja wa Mataifa iliyofanyika nchini mwezi Julai 2019. Lengo la ziara hiyo, lilikuwa ni kukusanya maoni kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali ya usalama nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kubaini mahitaji halisi ya Misheni ya Umoja wa Mataifa ya Ulinzi wa Amani (MONUSCO).

235. *Mheshimiwa Spika*, ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Azimio Na. 2463 (2019) la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linalomtaka Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kufanya mapitio ya muundo na majukumu ya MONUSCO kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wake. Taarifa ya ziara hiyo ilitumiwa na Umoja wa Mataifa kuongeza muda kwa MONUSCO kuendelea kuimarisha usalama katika eneo la Maziwa Makuu. Tanzania ilishiriki kikamilifu kwenye ziara hiyo kwa kuwa ni mdau muhimu katika misheni ya kulinda amani nchini DRC.

8.2 Kufuatilia na Kusimamia Utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa

236. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara iliratibu na kushiriki

katika majadiliano na kusimamia uwekwaji wa saini wa Mikataba na Hati za Makubaliano zifuatazo:

- a) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika Ukuzaji wa Biashara Ndogo na za Kati iliyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;
- b) Hati ya Makubaliano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika masuala ya Uchumi, Biashara na Uwekezaji iliyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;
- c) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika masuala ya Wanawake, Jinsia na Maendeleo ya Jamii iliyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;
- d) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika masuala ya Mashauriano ya Kidiplomasia iliyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;

- e) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zimbabwe katika sekta ya Utalii iliyosainiwa mwezi Julai 2019 jijini Harare, Zimbabwe;
- f) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda katika sekta ya Kilimo iliyosainiwa mwezi Septemba 2019 jijini Dar es Salaam;
- g) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda katika masuala ya Magereza iliyosainiwa mwezi Septemba 2019 jijini Dar es Salaam;
- h) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda katika masuala ya Uhamiaji iliyosainiwa mwezi Septemba 2019 jijini Dar es Salaam;
- i) Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi kuhusu msaada wa matengenezo na upanujaji wa Hospitali

ya Wete, Pemba iliyosainiwa mwezi Septemba 2019 Abu Dhabi; na

- j) Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Rwanda katika Sekta ya Usafiri wa Anga uliosainiwa mwezi Desemba 2019 Aqaba, Jordan;
- k) Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Mauritius katika Sekta ya Usafiri wa Anga uliosainiwa mwezi Desemba 2019 Aqaba, Jordan;
- l) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Namibia katika sekta ya Utalii iliyosainiwa mwezi Desemba 2019 jijini Dar es Salaam;
- m) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Namibia katika masuala ya Utamaduni iliyosainiwa mwezi Desemba 2019 jijini Dar es Salaam;

- n) Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Namibia katika maendeleo ya Vijana iliyosainiwa mwezi Desemba 2019 jijini Dar es Salaam; na
- o) Mkataba wa Ushirikiano wa kitaalam kati ya Hospitali ya Benjamin Mkapa na Wizara ya Afya ya Serikali ya Watu wa Cuba kuhusu kuwaleta madaktari bingwa nchini uliosainiwa mwezi Januari 2020 Jijini Dodoma.

237. *Mheshimiwa Spika*, Mikataba na Hati hizo za Makubaliano zilizosainiwa zinalenga kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na nchi marafiki pamoja na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Tanzania itanufaika na fursa zilizopo katika maeneo yaliyolengwa katika mikataba pamoja na makubaliano hayo.

8.3 Kuratibu Mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano na Kufuatilia Utekelezaji wa Makubaliano

238. *Mheshimiwa Spika*, mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano ni kiungo muhimu katika kuimarisha uhusiano na

ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi marafiki. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano iliyofanyika kama ifuatavyo:

Zimbabwe

239. Mheshimiwa Spika, mwezi Julai 2019, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Nane wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Zimbabwe uliofanyika Harare, Zimbabwe. Katika Mkutano huo, Tanzania na Zimbabwe zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya viwanda, biashara, uwekezaji, fedha, madini, uchukuzi, kilimo, mazingira na utalii. Aidha, Hati tano za Makubaliano ya Ushirikiano zilisainiwa kuhusu mashauriano ya kidiplomasia; utalii; ukuzaji wa biashara ndogo na za kati; viwanda na biashara; wanawake, jinsia na maendeleo ya jamii.

Uganda

240. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Tatu wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Uganda uliofanyika mwezi Septemba 2019 jijini Dar es Salaam. Katika Mkutano huo, Tanzania na

Uganda zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya biashara, uchukuzi, kilimo, nishati, ulinzi na usalama. Aidha, wakati wa Mkutano huo Tanzania na Uganda zilisaini hati tatu za makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya kilimo, mageza na uhamiaji.

Namibia

241. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Namibia uliofanyika mwezi Desemba 2019 jijini Dar es Salaam. Katika Mkutano huo, Tanzania na Namibia zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya mifugo, uvuvi, elimu, kilimo, biashara, utalii, utamaduni na vijana. Hati za makubaliano ya ushirikiano zilizosainiwa kwenye Mkutano huo ni katika masuala ya utalii, utamaduni na maendeleo ya vijana.

8.4 Masuala ya Diplomasia, Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli

8.4.1 Kuratibu Ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Nje ya Nchi

242. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuandaa na kuratibu ziara mbalimbali za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi kama ifuatavyo:

- a) Ziara ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Zambia wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani Tunduma/Nakonde mwezi Oktoba 2019;
- b) Ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Niger akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika, mwezi Agosti 2019;

- c) Ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Botswana akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Sherehe za kuapishwa Rais wa Botswana, Mheshimiwa Dkt. Mokgweetsi E. K. Masisi, zilizofanyika mwezi Novemba 2019;
- d) Ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ethiopia akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 33 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, mwezi Februari 2020;
- e) Ziara ya Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) mwezi Septemba 2019;

- f) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Maadhimisho ya Ukombozi wa Rwanda mwezi Julai 2019;
- g) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Misri mwezi Julai 2019;
- h) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Japan akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa *Tokyo International Conference on African Development* (TICAD VII) mwezi Septemba 2019;
- i) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Urusi akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John

Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika na Urusi mwezi Oktoba 2019;

j) Ziara ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Azerbaijan akimwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote mwezi Oktoba 2019; na

k) Ziara za Waheshimiwa Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye mikutano mbalimbali nje ya nchi.

8.4.2 Kuratibu Ziara za Viongozi wa Kitaifa na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa kutoka Nje ya Nchi

243. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu ziara za Viongozi wa Mataifa mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa waliokuja Tanzania kushiriki katika

mikutano, makongamano na kutekeleza majukumu mbalimbali ya kitaifa kama ifuatavyo:

- a) Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Uhuru Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya mwezi Julai 2019;
- b) Ziara za kikazi za Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda mwezi Julai 2019 na Septemba 2019;
- c) Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Cyril Matamela Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini mwezi Agosti 2019;
- d) Ziara za kikazi za Wakuu wa Nchi na Serikali na Wawakilishi pamoja na Wakuu wa Mashirika mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa katika Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC mwezi Agosti 2019;
- e) Ziara ya Mheshimiwa Edgar Chagwa Lungu, Rais wa Jamhuri ya Zambia wakati wa Uzinduzi wa Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani Tunduma/Nakonde mwezi Oktoba 2019; na

f) Ziara za wajumbe maalum kutoka nchi mbalimbali kuja kuwasilisha ujumbe maalum kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

8.5 Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli

244. Mheshimiwa Spika, ili kunufaika ipasavyo na diplomasia ya uchumi, nchi yetu imeendelea kufungua balozi katika nchi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali imefungua Ubalozi mpya Windhoek nchini Namibia. Hatua hii imeiwezesha nchi yetu kufungua balozi mpya nane katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Balozi nyingine zilizofunguliwa katika kipindi hicho zipo katika nchi za Algeria, Uturuki, Sudan, Korea Kusini, Israel, Qatar na Cuba. Kwa misingi hiyo, Tanzania ina jumla ya Balozi 43 na Konseli Kuu tatu zilizopo katika nchi mbalimbali duniani.

245. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma za kikonseli kama ifuatavyo:

- a) Kurahisisha upatikanaji wa viza kwa Maafisa na Watendaji wa Serikali, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Waheshimiwa Wabunge na Taasisi nyingine zinazostahili huduma hiyo. Aidha, Balozzi zetu zimeendelea kutoa viza kwa raia wa nje wanaoitembelea Tanzania;
- b) Kuratibu uwasilishaji wa Hati za Utambulisho kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka kwa Mabalozzi wa nchi za Saharawi, India, Zimbabwe, Angola, Denmark, Finland, Rwanda, Umoja wa Ulaya, Ujerumani, Algeria, Singapore, Qatar, Ureno, Austria, Ufilipino, Jamaica, Venezuela, Israel, Ghana na Djibouti;
- c) Kupokea hati za utambulisho kutoka kwa Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umoja wa Mataifa ambao ni Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UNRC); Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF); na Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR);

d) Kushirikiana na mamlaka nyingine kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili Watanzania waishio nje ya nchi; na

e) Kutatua changamoto na kulinda maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini.

8.6 Ushirikishwaji wa Watanzania wanaoishi ughaibuni

246. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwashirikisha Watanzania wanaoishi ughaibuni (Diaspora) katika kuchangia maendeleo ya nchi yao. Mwezi Septemba 2019 Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya kampuni ya *AVZ Minerals* kutoka Australia iliyofanyika jijini Dar es Salaam. Ziara hiyo ilitokana na jitihada za *Diaspora* wanaoishi nchini Australia za kuhamasisha wawekezaji kutoka nchini humo kuja kuwekeza nchini. Kampuni hiyo inayomiliki migodi ya madini ya *Lithium* iliyopo katika eneo la Manono nchini DRC inatarajia kutumia bandari ya Dar es Salaam kupitia reli ya TAZARA na Reli ya Kati (TRC) kusafirisha madini hayo nje ya nchi.

247. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya kampuni ya *Eco Systems International* ya Ireland iliyofanyika mwezi Oktoba 2019. Kampuni hiyo inajishughulisha na utengenezaji wa vifaa vya kupunguza gesi ya ukaa hususan ile inayotokana na matumizi ya vyombo vya moto, imeonesha nia ya kuwekeza nchini. Ujio wa kampuni hiyo ni matokeo ya kongamano la *Diaspora* lililoratibiwa na Wizara lililofanyika mwezi Aprili 2019 nchini Sweden. Wizara kwa kushirikiana na sekta husika inaendelea kuchambua maombi ya kampuni hiyo kwa ajili ya kufanikisha uwekezaji huo.

248. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya timu ya matabibu na wataalam wengine wa afya kutoka Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchini Uingereza ijulikanayo kama *The Tanzania - UK Healthcare Diaspora Association (TUHEDA)* iliyofanyika nchini mwezi Novemba 2019. Ujumbe huo ulitembelea hospitali ya Tumbi iliyopo Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani na kutoa msaada wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na sanamu ya vitendo vyenye thamani ya **Shilingi 100,000,000** na vitabu vya sayansi ya afya vyenye thamani ya **Shilingi 30,000,000**.

249. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kushiriki katika Kongamano la Sita la Watanzania wanaoishi nje ya nchi lililofanyika Zanzibar mwezi Desemba 2019. Kongamano hilo lilifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kushirikisha wajumbe wapatao 300 wakiwemo *Diaspora* kutoka nchi mbalimbali, viongozi wa Serikali na sekta binafsi. Kauli mbiu ya Kongamano hilo ilikuwa “Kuendeleza Ushirikiano Uliojengwa na *Diaspora* na Wawekezaji Kama Wadau wa Maendeleo Nchini”.

250. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na hatua za kukusanya taarifa na kufanya uchambuzi kwa ajili ya kuandaa mwongozo wa kisera wa kuimarisha ushiriki wa Watanzania waishio ughaibuni katika mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo hapa nchini. Hatua iliyofikiwa sasa ni uchambuzi wa masuala ya kisheria na kitaasisi, ushiriki wa sekta binafsi, pamoja na uwezo na utayari wa Watanzania hao kushiriki katika kuleta maendeleo ya nchi yao.

251. Mheshimiwa Spika, uchambuzi huo umebaini kuwa ukosefu wa takwimu za Watanzania waishio ughaibuni unailazimu Wizara kuendelea kuboresha kanzidata ya takwimu

zitakazoonesha sifa na uwezo wao kwanza kabla ya kutunga Sera ili matamko ya Sera hiyo yawe yamezingatia uhalisia uliopo. Wakati Wizara inaendelea kuboresha kanzidata hiyo, masuala ya Diaspora yatajumuishwa kwenye rasimu ya Sera ya Mambo ya Nje.

8.7 Elimu kwa Umma

252. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kuandaa makala, majarida, vipeperushi na mikutano na vyombo vya habari. Njia hizo zimewasaidia wadau kunufaika na fursa za masomo, ajira, masoko, uwekezaji, na utalii. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya fursa zitokanazo na Jumuiya ya Afrika Mashariki; Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika pamoja na jumuiya nyingine za Kikanda na Kimataifa.

253. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Wizara ilitoa mafunzo kwa waandishi wa habari 60 kuhusu namna ya kuripoti mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayofanyika nchini na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania kupitia diplomasia ya mikutano. Aidha, Wizara

iliratibu ushiriki wa mabalozi wa Tanzania nje katika vipindi mbalimbali vya redio na televisheni kwa lengo la kuelezea namna wanavyotekeleza diplomasia ya uchumi.

8.8 Mpango Mkakati wa Wizara kwa Kipindi cha Mwaka 2020/2021- 2024/2025

254. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Wizara imekamilisha Mpango Mkakati wa utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha Miaka Mitano (2020/2021- 2024/2025). Mpango huo umezingatia mabadiliko ya muundo wa Wizara pamoja na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yanayoendelea ndani na nje ya nchi.

8.9 Utawala na Maendeleo ya Watumishi

255. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi. Wizara ina jumla ya watumishi 439 wa kada mbalimbali. Kati ya watumishi hao, watumishi 338 wapo Makao Makuu ya Wizara na watumishi 101 wapo kwenye Balozi zetu nje. Katika kuimarisha utendaji kazi wa Wizara, masuala mbalimbali yanayohusu utawala na maendeleo ya watumishi yameendelea kusimamiwa kama ifuatavyo: -

8.9.1 Uteuzi wa Viongozi

256. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Balozi Kanali Wilbert Augustin Ibuge kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Vilevile, Mheshimiwa Rais aliwateua Mabalazi 17 ambapo 14 kati yao wanaiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali duniani na watatu ni Mabalazi wanaofanya shughuli zao hapa nchini. Naomba kutumia fursa hii kuwapongeza kwa uteuzi huo na kuwataka waendeleo kuchapa kazi kwa bidii, uzalendo na weledi mkubwa.

8.9.2 Mafunzo

257. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo jumla ya watumishi 93 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Watumishi waliohudhuria mafunzo ya muda mrefu ni 51 na mafunzo ya muda mfupi ni 42. Aidha, katika kipindi hiki, Wizara iliratibu upatikanaji wa nafasi 578 za mafunzo kutoka nchi

marafiki 20, kati ya nafasi hizo mafunzo ya muda mfupi ni 225 na ya muda mrefu ni 134. Nafasi hizo zilitangazwa kwa umma wa Watanzania kupitia vyombo vya habari ili kunufaika na fursa hizo za mafunzo.

8.9.3 Upandishaji Vyeo Watumishi

258. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, watumishi 19 walipandishwa vyeo kwa mserekeo. Kati ya watumishi hao, watano walipandishwa kuwa Maafisa Mambo ya Nje Wakuu Daraja la I na watumishi 14 walipandishwa kuwa Maafisa Mambo ya Nje Wakuu Daraja la II.

8.9.4 Uhamisho

259. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, watumishi 15 walihamishwa kwenda Wizara na Taasisi nyingine za Serikali na watumishi 26 walihamia Wizarani kutoka Wizara na Taasisi nyingine za Serikali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma. Aidha, watumishi 35 walirejeshwa kutoka balozi mbalimbali za Tanzania nje ya nchi baada ya kumaliza muda wao wa utumishi ubalozini. Hadi sasa watumishi 20 wamepelekwa Balozini

kwa lengo la kuimarisha utendaji. Wizara inaendelea na taratibu za kuwapeleka watumishi zaidi katika Balozzi zetu.

8.9.5 Umiliki wa majengo

260. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati majengo yake ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Miaka 15 (2017/2018-2031/2032) wa Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini. Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea kutekeleza mpango huo kwa kukarabati majengo ya Balozzi za Tanzania nje ikiwemo ukarabati wa Jengo lenye Ghorofa tisa kwenye Ubalozzi wetu jijini Maputo kwa ajili ya Ofisi na Makazi ya Watumishi wa Ubalozzi. Kwa sasa Tanzania inamiliki majengo 106 pamoja na viwanja 12.

8.10 Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi zilizo Chini ya Wizara

8.10.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara

261. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ilipangiwa bajeti ya maendeleo ya Shilingi **4,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo ndani na nje ya nchi.

262. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Wizara imepokea kiasi cha **Shilingi 487,905,996.40** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango sawa na asilimia 12.2 ya fedha zilizoidhinishwa. Tayari ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania Ottawa nchini Canada umeanza ambao utagharimu **Shilingi 150,000,000.00**. Vilevile, **Shilingi 337,905,996.40** zinatumiwa katika ujenzi wa vyumba vya madarasa unaoendelea kwenye Chuo cha Diplomasia.

8.10.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara

263. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kuzisimamia taasisi za Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC); Chuo cha Diplomasia (CFR); na Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (APRM) katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:

8.10.2.1 Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC)

264. *Mheshimiwa Spika*, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha kinaendesha biashara ya kumbi za mikutano; na upangishaji wa ofisi na nyumba za makazi. Aidha, kituo kinatoa huduma ya afya kupitia hospitali yake iliyopo jijini Arusha. Kituo hicho kinajiendesha kwa faida na kinatoa gawio kwa Serikali kwa mujibu wa maelekezo ya Msajili wa Hazina.

265. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuzingatia sheria iliyoanzisha Kituo, AICC inatekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2017/18-2021/2022). Mpango huo unaainisha dira na dhima ya Kituo

husususan katika kuitangaza nchi yetu katika nyanja ya utalii wa mikutano na matukio (business tourism) ambayo inajulikana kama “MICE” (Meetings, Incentive travel, Conferences, Exhibition/Events).

266. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Kituo kimepanga kukusanya mapato ya **Shilingi 16,313,716,937.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,603,468,044.00** ni kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani na **Shilingi 710,248,893.00** zitatokana na mkopo.

267. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 Kituo kimekusanya mapato ya **Shilingi 11,815,516,916** sawa na asilimia **72** ya lengo la mwaka. Mapato hayo yalitokana na:

a) Huduma za kumbi za mikutano (AICC na JNICC) **Shilingi 4,986,883,072** sawa na asilimia **123** ya lengo la **Shilingi 4,047,496,666**;

b) Upangishaji wa ofisi na nyumba za kuishi **Shilingi 3,514,566,238** sawa na asilimia **108** ya lengo la **Shilingi 3,264,037,760**; na

c) Huduma za hospitali **Shilingi 3,314,067,603** sawa na **asilimia 107** ya lengo la **Shilingi 3,090,777,602**.

268. Mheshimiwa Spika, vilevile katika kipindi cha 2019/2020, Kituo kilitoa **Shilingi 200,000,000** kama gawio la awali kwa Serikali. Pia, katika kipindi husika hadi tarehe 30 Aprili 2020, Kituo kilifanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

- i) Kuhudumia mikutano 144 ya Kitaifa na 24 ya Kimataifa ambayo ilileta washiriki 52,359 wa Kitaifa na 11,174 wa Kimataifa na kutoa huduma mbalimbali za afya kwa wagonjwa wapatao 80,190;
- ii) Kuweka matangazo ya vivutio mbalimbali vya utalii kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi la Taifa, Bodi ya Utalii Tanzania, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro;
- iii) Kufanya matengenezo makubwa ya Kituo cha JNICC na AICC (Ukumbi wa Simba);

- iv) Kuhuisha mifumo ya kielektroniki na kimenejimenti ya usimamizi wa taarifa katika nyanja za uhasibu, miliki na uendeshaji wa hospitali;
- v) Kukamilisha rasimu ya usanifu wa michoro ya mradi mkubwa wa *Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC)*;
- vi) Kukarabati majengo mawili yaliyopo viwanja Na. 46 na 47 *Old Moshi Road*; na
- vii) Kukarabati mtaro mkubwa wa maji katika miliki ya Kaloleni. Ukarabati huu utazuia mafuriko yaliyokuwa yakiingia kwenye baadhi ya nyumba za makazi.

8.10.2.2 Chuo cha Diplomasia

269. *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya Chuo ni kutoa mafunzo na kufanya tafiti katika masuala ya diplomasia; uhusiano wa kimataifa; stratejia na usuluhishi wa migogoro; na ujenzi wa amani. Lengo ni kukifanya Chuo kuwa Taasisi iliyobobea katika elimu ya juu na ushauri katika nyanja hizo.

270. *Mheshimiwa Spika*, Chuo kimeanza kutoa mafunzo ya lugha ya Bahasa (Indonesia)

baada ya kusaini makubaliano na Ubalizi wa Indonesia mwezi Agosti 2019. Kuanza kwa mafunzo hayo kumeongeza idadi ya lugha za kigeni zinazofundishwa kufikia nane. Lugha nyingine zinazofundishwa ni Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kiingereza, Kichina, Kikorea na Kireno. Aidha, Chuo kipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mtaala wa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni.

271. Mheshimiwa Spika, vilevile, Chuo kimefanikiwa kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali kwa mwaka wa masomo 2019/2020 kutoka wanafunzi 1,029 mwaka 2018/2019 hadi wanafunzi 1,280 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la **asilimia 24.**

272. Mheshimiwa Spika, vilevile Chuo kimekuwa na utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwagharamia kwenye mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani mbalimbali kulingana na uhitaji na umuhimu. Hadi kufikia mwezi Desemba 2019 mtumishi mmoja wa ngazi ya shahada ya uzamivu alihitimu masomo yake na kuongeza idadi ya wahitimu katika ngazi hiyo kufikia saba; na watumishi wanne wa shahada ya uzamili walihitimu masomo

yao na kufanya idadi ya wahitimu wa ngazi hiyo kufikia 44.

273. Mheshimiwa Spika, Mkataba wa mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa ulisainiwa kati ya Chuo na mkandarasi *Ms. Casco Construction Limited* na utekelezaji ulianza rasmi tarehe 16 Desemba, 2019. Mradi huu utagharimu kiasi cha **Shilingi 3,937,247,328.00** ambapo hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020 Chuo kilipokea kiasi cha **Shilingi 337,905,996.40** na kumlipa mkandarasi malipo ya awali kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

274. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Chuo kiliidhinishiwa **Shilingi 4,507,986,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,507,986,000** kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Chuo kilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 1,545,001,530** kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani.

275. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2020, Chuo kilipokea Shilingi 2,641,642,486 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,637,072,490 ni kwa ajili ya

mishahara, Shilingi 666,664,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 337,905,996 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa. Aidha, Chuo kilikusanya jumla ya Shilingi 1,510,514,650 sawa na asilimia 97 ya lengo la mwaka la Shilingi 1,545,001,530.

8.10.2.3 Mpango wa Afrika wa Kujitathmini Kiutawala Bora

276. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2019/2020, APRM Tanzania iliendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango Mkakati wake wa Miaka Mitano (2017/2018 - 2021/2022) unaohuishwa kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya kila mwaka. Malengo yaliyotekelezwa kwa kipindi hiki ni kama ifuatavyo:

- a) Kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM Tanzania;
- b) Kuimarisha uhamasishaji wa mawasiliano kwa umma; na
- c) Kuhakikisha kuwa shughuli za APRM Tanzania zinakuwa endelevu.

277. Mheshimiwa Spika, APRM Tanzania imekamilisha rasimu ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM inayohusu maeneo ya Siasa na Demokrasia, Usimamizi wa Uchumi, Uendeshaji wa Kampuni za Biashara na utoaji wa huduma za jamii. Mara baada ya taarifa hii kuridhiwa na wadau itawasilishwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika.

278. Mheshimiwa Spika, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za APRM - Tanzania kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni **Shilingi 948,012,866**. Fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 638,240,000** sawa na **asilimia 67**.

9.0 CHANGAMOTO ZILIZOPO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

279. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na kuwepo mafanikio ya kiutendaji, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:

- i) Kuongeza idadi ya watumishi ili kukidhi mahitaji yanayotokana na wingi wa majukumu ya Wizara;

- ii) Kuendelea kuongeza idadi ya magari ili kukidhi mahitaji ya Wizara;
- iii) Kasi ndogo ya sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki na masoko ya kimataifa; na
- iv) Uelewa mdogo wa Watanzania kuhusu masuala na fursa zitokanazo na Mtangamano wa Kikanda.

280. *Mheshimiwa Spika*, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua zifuatazo:

- i) Kuendelea kuwasiliana na mamlaka husika kwa ajili ya kupatiwa vibali vya ajira mpya na kujaza nafasi zilizo wazi;
- ii) Kuendelea kutoa kipaumbele cha upatikanaji wa magari katika bajeti ya Wizara;
- iii) Kuendelea kushirikiana na Taasisi za sekta binafsi, asasi za kiraia na vyombo vya habari katika kutoa elimu kwa umma juu ya fursa mbalimbali zitokanazo na ushiriki

wetu katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa; na

- iv) Kuendelea kuhamasisha umma kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza katika nchi mbalimbali, Jumuiya za Kikanda na Kimataifa.

10.0 SHUKRANI

281. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuwa hii ni Hotuba yangu ya mwisho ya Bajeti katika Bunge la 11, kwa mara nyingine tena, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu iliyomfanya kuiteua kuwa Mbunge tarehe 22 Oktoba, 2018 na kuiteua kuwa Waziri wa Katiba na Sheria nafasi ambayo nilihudumu hadi tarehe 3 Machi, 2019 aliponiteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kutokana na imani yake kwangu nimeweza kushirikiana na viongozi na watumishi wa Wizara zote mbili nilizohudumu kutekeleza yale yote ambayo Viongozi wangu wakuu wameniagiza. Nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa fursa ambayo sikustahili kuitumikia nchi yangu katika nafasi hii

kubwa kabisa. Nashukuru kuwa nimeweza kutoa mchango wangu katika maendeleo ya nchi yetu na katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 – 2020.

282. *Mheshimiwa Spika*, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitatoa shukrani zangu za kipekee kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar; na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yao ambayo ilikuwa ni nguzo muhimu kwenye utekelezaji wa majukumu yangu katika nafasi zote zilizowahi kushika. Nalishukuru pia Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa niliopatiwa katika kulitumikia Taifa na kuchangia katika kufanikisha maendeleo makubwa yaliyopatikana katika Serikali ya Awamu ya Tano.

283. *Mheshimiwa Spika*, naomba nitumie fursa hii kwa namna ya pekee kuwashukuru Mabalizi na Wawakilishi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa pamoja na Mashirika mengine ya Kimataifa hapa nchini kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kupitia nchi na mashirika yao

kufanikisha mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

284. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kupata mafanikio makubwa kutokana na mchango wa wadau na Washirika wa Maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za kimataifa, kikanda na kitaifa na sekta binafsi. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi za Algeria, Australia, Austria, Brazil, Brunei, Canada, China, Cuba, Denmark, Ethiopia, Finland, Hungary, Italia, Iran, Ireland, Indonesia, India, Israel, Jamhuri ya Korea, Japan, Kuwait, Malaysia, Malta, Marekani, Mexico, Misri, Morocco, New Zealand, Norway, Oman, Pakistan, Poland, Qatar, Romania, Saudi Arabia, Singapore, Sri Lanka, Sweden, Sudan, Thailand, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani, Urusi, Uswisi, Uturuki, Ureno, Umoja wa Falme za Kiarabu, Venezuela na Viet Nam kwa kuchangia kwenye jitihada za maendeleo ya nchi yetu.

285. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani pia kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika;

Umoja wa Ulaya; *African Capacity Building Foundation*; Benki ya Dunia; Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); *Investment Climate Facility for Africa*; Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa; Shirika la Mpango wa Chakula Duniani; Ofisi ya Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN RCO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Ukimwi (UNAIDS); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Shirika la Afya Duniani (WHO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR); Shirika la Kazi Duniani (ILO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Uhamaji (IOM); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP); Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD); Mfuko wa Kukuza Mtaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughukia Maendeleo ya Viwanda (UNIDO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UN WOMEN); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo

(UNCTAD); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Madawa ya Kulevyu na Uhalifu (UNODC).

286. Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashukuru *TradeMark East Africa*; Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya; *The Association of European Parliamentarians with Africa*; Mfuko wa Dunia wa Wanyama Pori; *The Belinda and Bill Gates Foundation*; *Global Fund*; *International Committee of the Red Cross*; *International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies*; *Medecins Sans Frontieres* pamoja na Mifuko na Mashirika mbalimbali ya misaada.

287. Mheshimiwa Spika, ninayashukuru pia Mashirika na Taasisi zisizo za Kiserikali, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu, Vyombo vya Habari, Taasisi za Dini na wadau wote ambao wamekuwa wakishirikiana na mimi pamoja na Wizara nzima kwenye utendaji wetu wa kazi. Ni dhahiri kuwa ushirikiano wao umeisaidia Serikali katika kutimiza baadhi ya malengo yake.

288. Mheshimiwa Spika, kwa moyo mkunjufu, napenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa

Wizara na Taasisi zake kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Balozi Kanali Wilbert Augustin Ibuge, Katibu Mkuu; Balozi Ramadhan Muombwa Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu; Mabalazi wa Tanzania Nje ya Nchi; Wakuu wa Idara na Vitengo; Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wengine wote kwa weledi, umahiri na ufanisi wao katika kunisaidia kutekeleza majukumu yangu ya kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu.

289. Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa, napenda kumshukuru mke wangu mpendwa Dkt. Amina M. M. Kabudi na familia yangu kwa ujumla kwa uvumilivu wao na kuwa karibu na mimi wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu niliyopewa na Mheshimiwa Rais ambayo wakati mwingine yanani lazimu kuwa mbali nao kwa muda mrefu.

11.0 MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

290. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na masuala mengine, Wizara imeweka kipaumbele katika kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i) Kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuvutia wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nje, kuvutia watalii, kutafuta misaada na mikopo yenye masharti nafuu, kutafuta fursa za mafunzo, kushiriki katika Jumuiya za Kikanda kwa lengo la kuongeza ajira na masoko ya bidhaa za Tanzania nje;
- ii) Kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje 2020, Sera hiyo itazingatia mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii;
- iii) Kuboresha Kanzidata ya Diaspora itakayotoa taarifa itakayosaidia kuandaa mwongozo wa namna ya kuwashirikisha Diaspora wa Tanzania kuchangia katika maendeleo ya nchi yao;

- iv) Kuendelea kutumia Balozi zetu kutafuta mitaji ya uwekezaji, masoko na kuhamasisha Diaspora kuchangia kwenye maendeleo ya nchi kwa kutangaza vyema miradi ya vipaumbele na vivutio vinavyotolewa na Serikali katika maeneo yao ya uwakilishi;
- v) Kuendelea na utafutaji wa masoko mapya ya bidhaa za Tanzania nje kwa kuendelea kuhamasisha Taasisi za Serikali zinazohusika na biashara kushirikiana na sekta binafsi kushiriki katika maonesho mbalimbali ya Kimataifa ambayo yanatoa fursa kwa nchi mbalimbali kutangaza bidhaa zake pamoja na kujifunza teknolojia na mbinu za kisasa zitakazoboresha bidhaa zetu;
- vi) Kuendelea kutekeleza Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake;
- vii) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini kwa Afrika wa mwaka 2015 - 2020 na Mkakati wa Kuendeleza Viwanda wa Jumuiya ya

Maendeleo Kusini mwa Afrika wa mwaka
2015 – 2030;

- viii) Kushiriki katika juhudi za kuleta amani, usalama na kukuza demokrasia kwenye Jumuiya za Kikanda ambazo nchi yetu ni mwanachama;
- ix) Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya fursa zitokanazo na Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za Kikanda;
- x) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara, Balozi na Taasisi zilizopo chini ya Wizara; na
- xi) Kuendelea kusimamia rasilimali watu; rasilimali fedha na rasilimali vitu vya Wizara na Balozi.

12.0 MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Afrika (APRM)

291. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, APRM inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

- i) Kuimarisha Tathmini za Utawala Bora za Mpango wa APRM ikiwa ni pamoja na kuhuisha mbinu za utafiti kwa kupitia upya hojaji ya APRM;
- ii) Kuboresha viashiria vya utafiti, kuzingatia matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa Mpango na kupanua wigo wa zana zinazotumika katika utafiti;
- iii) Kuratibu ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Wakala za Serikali katika kuandaa taarifa ya mwaka pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa mfumo madhubuti wa ufuatiliaji; na

- iv) Kuimarisha mawasiliano na utoaji taarifa kuhusu Mpango wa APRM kwa kuendelea kutekeleza Mpango wa Mawasiliano wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21.

Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC)

292. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, AICC inatarajia kukusanya mapato ya **Shilingi 16,701,559,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,001,559,000** ni kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani ambapo kituo cha Arusha kinatarajia kukusanya **Shilingi 12,785,009,000** na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kinatarajia kukusanya **Shilingi 3,216,550,000**. Aidha, mapato ya **Shilingi 700,000,000** yatatokana na mkopo kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa Hospitali ya AICC.

293. Mheshimiwa Spika, Kituo kinaendelea kufanya taratibu za kuwezesha ujenzi wa kituo mahsusi cha mikutano jijini Arusha kitakachoitwa *Mt. Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC)*. Kituo hicho kitakuwa kichocheo cha utekelezaji wa diplomasia ya mikutano ya kimataifa na maonesho hapa nchini.

Chuo cha Diplomasia

294. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Chuo kinatarajia kutekeleza masuala yafuatayo:

- i) Kutoa mafunzo ya mahusiano ya kimataifa na mbinu za kidiplomasia;
- ii) Kufanya utafiti kubaini mahitaji na changamoto katika fani za mahusiano ya kimataifa na mbinu za kidiplomasia;
- iii) Kutathmini matokeo ya mafunzo yaliyotolewa na mipango ya mafunzo kwa ujumla; na
- iv) Kutoa ushauri na huduma za kitaalamu kwa Serikali na Taasisi zake.

13.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

295. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 2,550,879,000** ikiwa ni maduhuli ya Serikali yatakayopatikana kutokana

na vyanzo vilivyopo Makao Makuu ya Wizara na katika Balizi za Tanzania nje. Vyanzo hivyo vya mapato vinajumuisha pango la nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi; kuthibitisha nyaraka; na mauzo ya nyaraka za zabuni.

296. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, Wizara imepangiwa bajeti ya **Shilingi 199,750,684,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 179,750,684,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zinazojumuisha **Shilingi 167,717,723,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 12,032,961,000** kwa ajili ya Mishahara; na **Shilingi 20,000,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

297. Mheshimiwa Spika, kati ya fedha za bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara, **Shilingi 800,000,000** ni kwa ajili ya Mpango wa Afrika wa Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM), **Shilingi 1,000,000,000** ni kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia, **Shilingi 1,272,000,000** ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na **Shilingi 168,200,000** ni kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika. Aidha, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 2,427,064,000** ni kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia.


298. Mheshimiwa Spika, katika fedha za bajeti ya Maendeleo, kiasi cha **Shilingi 20,000,000,000** kilichopangwa kwa mwaka wa fedha 2020/21, **Shilingi 1,800,000,000** ni kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Balozi na ofisi katika Ubalози wa Tanzania Moroni, Komoro; **Shilingi 3,694,439,655** ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na makazi ya Balozi wa Tanzania Muscat, Oman; **Shilingi 1,500,000,000** ni kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa viwanja vya Serikali vilivyopo Kigali, Maputo, Bujumbura, Riyadh na Lilongwe; **Shilingi 3,948,120,345** ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Ubalози na Kitega Uchumi katika Ubalози wa Tanzania Nairobi, Kenya; **Shilingi 2,280,000,000** ni kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi na kitega uchumi katika Ubalози wa Tanzania Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; **Shilingi 3,864,440,000** ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ofisi yaliyopo Ubalози wa Tanzania Washington D.C, Marekani; **Shilingi 275,000,000** ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya makazi ya Balozi na watumishi wa Ubalози wa Tanzania Harare, Zimbabwe; **Shilingi 260,000,000.00** ni kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania Kigali, Rwanda; na **Shilingi 2,378,000,000.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Chuo cha Diplomasia.

14.0 HITIMISHO

299. Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya **Shilingi 199,750,684,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 179,750,684,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 20,000,000,000** ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

300. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii adhimu kukushukuru tena wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

301. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.



Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa katika picha ya pamoja na Mabalazi wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali baada ya kuwaapisha Ikulu jijini Dar es Salaam mwezi Januari 2020.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akiwa katika picha ya pamoja na Mawaziri wa Mambo ya Nje wa nchi za Afrika na Nordic mara baada ya Mkutano wao uliofanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) jijini Dar es Salaam mwezi Novemba 2019.



Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Edgar Chagwa Lungu, Rais wa Jamhuri ya Zambia wakikata utepe kwenye uzinduzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) Tunduma/Nakonde mwezi Oktoba, 2019.



Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika kwa njia ya video mwezi Machi 2020.